

Tanzania yalipa mabilioni 'kujisogeza' kwa Trump

Uk.
6&7

● Ni karibu Shilingi bilioni nane

POLE SANA RAIS...




MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa, Jumatano - Septemba 9, 2026 alifika Kizimkazi, Zanzibar kwa ajili ya kumfariji Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kufiwa na mumewe, Hafidh Ameri Hassan. (Picha na Ikulu)

Dkt Nchimbi asubiri 'vumbi litue,' yuko salama

NI siku 19 sasa tangu aliyekuwa Makamu wa Rais, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi ajiuzulu wadhifa wake Agosti 25, 2026, huku...

Uk.
12



Jicho la Tai

Chacha, hata kutongozwa unaogopa?

PAUL Matiko Chacha, Katibu wa NEC, Oganaizesheni wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ametuachia mjadala ambao hata vikao vya chama vinaweza kuuhitaji...

Safu Uk. 5

DSE yavunja rekodi, mtaji wafika trilioni 40/-

Habari Uk. 16

ACT, CCM 'mwendomdu' maridhiano

RAIS wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi ameitangaza Kamati ya Pamoja ya Majadiliano...

Habari Uk. 28

Ushahidi wa simanzi kutoka kwa John Heche

Habari Uk. 22

Tafakuri ya Bagonza

Serikali haina na wala haiendi eda

Safu Uk. 10

Madhara kupanda mfumko wa bei 'yatokota'

Habari Uk. 18

■ Tahariri

Uchumi imara uonekane nyumbani

SERIKALI ina wajibu wa kufanya kila lina-lowezekana kudhibiti mfumuko wa bei, hasa kwa bidhaa na huduma ambazo wananchi huzihitaji kila siku.

Uchumi unaweza kukua kwenye takwimu, deni la taifa likaelezwa kuwa himilivu na mapato ya serikali yakaongezeka, lakini mafanikio hayo hayatakuwa na maana kubwa ikiwa mwananchi wa kawaida hawezi kumudu chakula, usafiri na mahitaji muhimu ya familia.

Bei za unga, mchele, sukari, mafuta ya kupikia, maharage, na mboga zinapopanda, athari zake huingia moja kwa moja katika kila nyumba.

Wanaoathirika zaidi ni wafanyakazi wenye mishahara midogo, wakulima wenye mapato yasiyotabirika, wafanyabiashara wadogo, wastaafu na familia ambazo tayari zinahangai-ka kulipa kodi, ada na gharama za matibabu.

Vivyo hivyo, kupanda kwa bei ya petroli na dizeli hakuishii kwenye vituo vya mafuta. Gharama hizo husambaa katika uchumi mzima kupitia nauli, usafirishaji wa mazao, uzalishaji viwandani na bei ya bidhaa sokoni.

Dereva anapolipa zaidi kujaza mafuta, mfanyabiashara huongeza gharama ya bidhaa, na mzigo wa mwisho humwangukia mlaji.

Ndiyo maana serikali inapaswa kuwa na mkakati wa kudumu, badala ya kusubiri bei zipande ndipo ianze kutafuta suluhisho.

Inapaswa kuimarisha akiba ya chakula, kupunguza upotevu wa mazao, kuboresha maghala na barabara za vijijini, kudhibiti tozo zinazoongeza gharama za biashara na kuhakikisha ushindani wa haki sokoni.

Wafanyabiashara wanaotengeneza uhaba bandia au kupandisha bei bila sababu wanapaswa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Pia, uratibu kati ya serikali, Benki Kuu, wazalishaji na wasambazaji lazima uimarishwe ili sera za fedha na bajeti zisaidiane.

Taarifa za bei zikusanywe kwa wakati kati-ka mikoa yote, na msaada ulengwe kwa kaya

zilizo hatarini zaidi. Bila ufuatiliaji makini, walanguzi wanaweza kutumia misukosuko midogo kujipatia faida kubwa kwa maumivu ya wananchi wengi.

Kwa upande wa mafuta, serikali inapaswa kuendelea kuchunguza maeneo yanayoweza kupunguza gharama katika mnyororo wa uagizaji, uhifadhi na usambazaji.

Kodi na tozo zinapaswa kupimwa kwa uangalifu ili mapato ya serikali yasikusanywe kwa namna inayomnyima mwananchi uwezo wa kuishi. Hatua yoyote ya muda mfupi pia isiathiri fedha zinazohitajika kwa afya, elimu na huduma nyingine za msingi.

Pambazuko tunatambua kuwa baadhi ya bei huathiriwa na soko la dunia, thamani ya fedha, vita, hali ya hewa na gharama za usafirishaji, hata hivyo, sababu hizo hazipaswi kuwa kisingizio cha kudumu kwa serikali kukaa pembeni.

Serikali makini hutabiri misukosuko, huandaa kinga mapema na kuwasiliana kwa uwazi na wananchi.

Watanzania hawali takwimu za ukuaji wa uchumi wala hawaendeshi magari kwa taarifa za deni himilivu. Wanataka kuona uthabiti huo katika bei ya chakula, nauli, umeme, mafuta na uwezo wa mishahara yao kununua mahitaji.

Furaha ya taifa huanza pale familia inapoweza kula, kusafiri, kujiuguza na kuweka akiba bila kuingia katika madeni ya kudumu.

Serikali inapaswa kupima mafanikio yake kwa hali halisi ya maisha ya wananchi. Mfumuko wa bei unapodhibitiwa, kipato hulindwa, biashara hustawi na matumaini huongezeka. Huo ndio ukuaji wenye maana; ukuaji unaoshuka kutoka kwenye majedwali na kuingia jikoni, sokoni na mifukoni mwa Watanzania.

Ziara ya Kikwete Tabora... ■



Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa JMKE, Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete, akizungumza na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Tabora mwishoni mwa wiki baada ya kuwasili kwa ziara ya siku nne ya kutembelea na kukagua zahanti zilizojengwa kwa lengo la kusaidia juhudi za serikali kuboresha upatikanaji wa huduma za afya. (Na Mpigapicha Maalum).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mwandishi Mwandamizi	:	Andrew MSECHU	0769 415 815
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz

■ Dunia: Hapa na Pale


Tanuru la vifo vya wajawazito

WAJAWAZITO hawako salama nchini Kenya. Tayari wajawazito 22 wameripotiwa kufariki dunia kutokana na matatizo yanayohusiana na uzazi ndani ya wiki moja, huku mgomo wa wauguzi ukiendelea nchini humo.

Pamoja nao, watoto wachanga 44 wameripotiwa kupoteza maisha pamoja na watoto 130 waliofariki kabla au wakati wa kuzaliwa, hivyo kufichua janga jipya la kiafya linalokumba Kenya.

Wahudumu wa afya katika hospitali za umma, wamekuwa kwenye mgomo baridi wa kazi ulioanza Julai 29, 2026, na huenda hali ikawa mbaya zaidi iwapo madaktari nao watatekeleza tishio lao la kugoma.

Chanzo ni mzozo kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Pamoja wa Kazi wa mwaka 2017, marupurupu na ajira za kudumu kwa wahudumu wa Mpango wa Afya kwa Wote.



Wizi bandia wa 'nyeti' hatari

IMEBAINIKA kuwa madai ya uongo kuhusu wizi wa sehemu za siri yamesababisha vifo vya zaidi ya watu 80 kati ya Oktoba 2025 hadi Julai 2026.

Imeelezwa kuwa takwimu za polisi kutoka nchi sita za Afrika, zinaonyesha mauaji hayo yamechochewa na uvumi unaodai kuwa kuguswa tu na mtu asiyejulikana kunaweza kusababisha sehemu za siri za mwanaume kusinyaa au kutoweka.

Taarifa hizo potofu zimeenea kwa kasi kupitia mitandao ya kijamii, zikisababisha hofu, vurugu na mashambulizi ya umati, kutokana na watu kujitokeza na kupiga kelele kwamba wameibiwa sehemu za siri, hivyo kusukuma mashambulizi ya umati na kusababisha vifo.



'AI yahatarisha maisha ya watu'

TEKNOLOJIA ya akili mnemba (AI) inazidi kuzua mambo, huku mtafiti maarufu katika eneo hilo, Jacob Coxon akiibuka na kushutumu kampuni za Marekani kwa "kucheza na maisha ya watu." Anasema sasa mifumo ya kompyuta inayoundwa inatishia uwezo wa binadamu.

Coxon amekuwa mtafiti katika kampuni ya AI ya Anthropic nchini Marekani, lakini sasa amejuzulu, baada ya kuchapisha onyo kali kupitia mtandao wa X siku ya Jumanne wiki iliyopita, akisema kwa siku za usoni AI siyo tu itakuwa na uwezo wa kudukua kila kitu, bali pia itaweza "kuwa na mamlaka halisi kila mahali."

Mtafiti huyo ameeleza kuwa watengenezaji wa AI wanaunda mifumo ya kompyuta itakayokuwa na uwezo unaozidi ule wa binadamu, akisisitiza kuwa itafika wakati wa kutishia uhai wa watu kwani hawatawweza kudhibiti.

Mcheza kamari aduwaa!

MWANAMKE mmoja kutoka Maryland, Marekani, amekutana na muujiza baada ya kushinda mfululizo michezo ya kamari ya baha-ti nasibu, akitumia seti namba za aina moja kwa miaka 20.

Mwanamke huyo amesema amekuwa akitumia seti ileile ya namba katika kamari hiyo, akiwa amenunua tiketi tatu zenye namba hizohizo katika droo moja ya mechi tano za nyongeza na kujishindia jumla ya dola 150,000.

Mkazi huyo wa White Plains, aliwaambia maofisa wasimamizi wa kamari huko Maryland kwamba amekuwa akicheza kwa kutumia namba hizohizo tano za 'bonas' kwa kipindi cha miaka 20.

Na Mzee TAI



Jicho la Tai

Chacha, hata kutongozwa unaogopa?

PAUL Matiko Chacha, Katibu wa NEC, Oganaisesheni wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ametuachia mjadala ambao hata vikao vya chama vinaweza kuuhitaji; je, kutongozwa ni kosa la jinai, sifa ya kisiasa au dharura inayohitaji kituo cha polisi?

Kwa simulizi yake, mwanamke aliyemtaja kwa jina la Sophia alifikishwa polisi baada ya kumtumia ujumbe wa simu eti unaompongeza na zaidi sana kubeba maono kwamba “anamkubali sana.”

Chacha akadai kwamba mwanamama huyo alikuwa pia anampa ujumbe wa kumtaka kimapenzi.

Sasa hapo ndipo mimi, kwa uzee wangu, nikajiuliza; Chacha ana shida gani? Au alitaka “attention” kidogo, jina lake lipite kwenye vichwa vya habari na watu wajue kuwa Katibu wa Oganaisesheni ana mvuto unaovuka mipaka ya matawi ya CCM?

Nilipokuwa CCM, tena nikiwa kiongozi, nilitongozwa mara nyingi. Sikuwahi kuomba gari la polisi, kuandaa jalada wala kuita waandishi wa habari. Nilijua jibu fupi linatosha: “Asante kwa kunikubali, lakini nimeoa na sina nafasi.”

Chacha angeweza kufanya vivyo hivyo, ikiwa kweli ujumbe ulikuwa ombi la mapenzi tu. Kumkataa mtu hakuhitaji pingu; kunahitaji sentensi iliyo wazi.

Mwanamke kumweleza mwanaume kuwa anampenda siyo uhalifu moja kwa moja, kama ambavyo mwanaume kumtongoza mwanamke siyo tiketi ya moja kwa moja kwenda kituoni. Kinacholeta tatizo ni kulazimisha, kutishia, kutukana, kufuatilia au kuendelea kutuma ujumbe baada ya kukataliwa.

Hapo ndipo tunapaswa kuwa waangalifu. Hatujaonyeshwa ujumbe wote, idadi yake wala mazingira yake. Ikiwa kulikuwa na vitisho, ulaghai, lugha chafu au usumbufu wa kudumu, Chacha alikuwa na haki ya kutafuta msaada wa polisi.

Lakini kama ilikuwa meseji ya “nakukubali” au “ninakupenda,” basi kutumia polisi ni sawa na kuita zimamoto kwa sababu mshumaa umewaka mezani.



Huenda Sophia hakuvutiwa na sura pekee, labda aliona utendaji wa Chacha alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, akamkubali, kama CCM ilivyomuona na kumvuta makao makuu.

Mimi hapo nashangaa, badala ya Chacha kusoma pongezi iliyopitiliza, kiongozi wetu akaona vyema afungue jalada la uchunguzi.

Tena, cheo chake kinahusu oganaizesheni, kazi ya kuunganisha watu, kusikiliza hisia zao na kutatua mikwaruzano kwa hekima. Kama kila anayezidisha sifa au kutuma moyo kwenye simu atapelekwa polisi, basi vituo vitahitaji dawati maalumu la viongozi kuzongwa kimapenzi.

Somo hapa ni kubwa kuliko utani. Viongozi wana mamlaka, mitandao na vyombo vya dola vinavyowatii, wanapaswa kujizuia kuvigeuza kuwa kinga dhidi ya kila usumbufu mdogo wa maisha. Polisi wana majukumu mazito; hawapaswi kuwa kamati ya kuchuja watu wanawapenda viongozi.


Na pia, mipaka iheshimiwe. Kukubali utendaji wa kiongozi hakumpi mtu ruhusa ya kumsumbua bila mwisho, jibu la “hapana” linapaswa kutosha, lakini pia “hapana” isipotolewa, tukio la kawaida linaweza kuvikwa sare, likapandishwa kwenye gari la polisi na hata kuhukumu.

Kwa kumpeleka Sophia polisi kwa kutongoza tu, Chacha amefeli pakubwa katika kipimo cha busara.

Uongozi haupimwi kwa uwezo wa kuamuru, bali kwa kujua jambo gani linahitaji dola na lipi linahitaji ujumbe mmoja wa heshima.

■ Habari Kuu

Tanzania yalipa mabilioni 'kujisogeza' kwa Trump



Na Mwandishi WETU

SERIKALI kadhaa za Afrika, Tanzania ikiwemo, zinalipa mamilioni ya dola kwa kampuni za ushawishi nchini Marekani zenye uhusiano na mtandao wa kisiasa na kikazi wa Rais Donald Trump.

Lengo la malipo hayo ni kupata fursa kubwa zaidi ya kufikia na kujisogeza zaidi kwa Marekani; nchi tajiri zaidi kwa fedha, uchumi imara na nguvu kubwa za kijeshi.

Idara ya Haki ya Marekani – kupitia Sheria ya Usajili wa Mawakala wa Kigeni (FARA), inaitaja Tanzania na baadhi ya nchi za Afrika kwamba uhusiano wao na Marekani umetetereka baada ya kukumbwa na mwenendo wa kisiasa “ulioshindwa kuifurahisha Marekani.”

Pambazuko limebaini kuwa nchi hizo, pamoja na Tanzania ni Kenya, Nigeria, Rwanda, Mo-

rocco, Somalia na Angola, ambazo sasa zinalipa mabilioni ya shilingi “kuhuisha zaidi uhusiano na Marekani.”

Serikali za nchi hizo zinaelezwa kulipa kuanzia mamia ya maelfu hadi mamilioni ya dola, ili kupata “sikio la Ikulu ya Rais Donald Trump na Serikali ya Marekani.

Tanzania yajitosa zaidi

Gazeti la Pambazuko limeona sehemu ya maelezo ya taarifa inayotokana na mkataba ulioingwa na Tanzania - kupitia FARA, kuwa Tanzania imesaini mkataba na kampuni ya BGR Government Affairs wenye thamani ya dola za Marekani milioni tatu kupitia usajili namba 5430, uliotiwa saina Juni 18, 2026. Mkataba huo utadumu kwa miezi 12.

Malipo hayo ya dola za Marekani 250,000 (zaidi ya Shilingi milioni 650) kwa mwezi, yataigharimu Tanzania karibu Shilingi bilioni 8 kwa mwaka.

Hata hivyo, pamoja na kulipa mabilioni hayo kwa “kujiweka karibu na Ikulu ya Marekani,” Tanzania – kupitia mkataba huo, itafanya kazi karibu na kampuni moja ya ushawishi ya Hispania, Drift Advisors, ambayo imethibitika kuwa na “uzoefu kwa kazi za namna hiyo. Kufikia Ikulu ya White House ya Marekani.”

Kumbukumbu za FARA zinataja kampuni hiyo ya Hispania kama mpatanishi anayefanya kazi kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa pia mkataba mwingine wa Ervin Graves Strategy Group, ambao unaripotiwa kuwa na thamani ya dola za Marekani 45,000 (zaidi ya Shilingi milioni 117) kwa mwezi, hivyo kuifanya Tanzania kutumia takribani dola milioni nne (zaidi ya Shilingi bilioni 10.4) katika ushawishi nchini Marekani.

Habari Kuu ■

Tanzania yalipa...

Inatoka Uk. 6

Timu ya BGR inajumuisha viongozi wa zamani waliowahi kuteuliwa kushika nyadhifa za ngazi za juu katika Ikulu ya White House, Bunge la Marekani na idara pamoja na mashirika ya tawi la utendaji la serikali.

Mtaalamu wa Uchumi wa Diplomasia ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. Walter Nguma, anasema matumizi ya kampuni hizo kwa ajili ya kufanya ushawishi kwa serikali za mataifa makubwa ni njia ambayo imekuwa ikitumika kwa miaka mingi hasa pale inapotokea kwamba nchi haina namna ya kuji-saidia kuwafikia wahusika moja kwa moja.

Hata hivyo, Dkt. Nguma anaonya kuwa njia hii siyo nzuri kwa sababu ni kiashiria cha kuzorota kwa wenye majukumu ya kuimarisha diplomasia baina ya nchi.

Anasema nchi inapoanza kutumia kampuni hizo siyo ishara nzuri kwa sababu katika hali ya kawaida nchi inatakiwa kutumia balozi zake katika nchi husika ambazo zina maofisa ambao wanalipwa mishahara na kutengewa kasma kwa ajili hiyo.

“Hii siyo ishara nzuri kwa diplomasia ya kisiasa na kiuchumi kwa kuwa inaonyesha kutowajibika ipasavyo na ni namna ya matumizi yasiyo sahihi ya fedha za umma kwa sababu lazima uainishe kwamba unatumia kampuni hizo ili kusaidia nini, nchi inanufaika vipi kwa hatua hiyo...”

“Hii inaingiza nchi katika kutumia utaratibu usiokuwa sahihi wa matumizi ya fedha za umma suala ambalo ni hatari katika uwajibikaji...”

“Ila inaweza kuwa jambo zuri kwa upande mwingine hasa nchi inapoonza kwamba haiwezi kufikia malengo katika eneo hilo kwa kutumia jitihada zake binafsi na inaonekana kuwa Tanzania imelazimika kuingia katika utaratibu huo hasa kutokana na mbinyo unaotokana na yale yaliyotokea katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025,” anasema.

Alisema kampuni hizo zipo katika nchi nyinigi zikiwemo Uingereza, mataifa mengine ya Ulaya na hata Urusi, ambapo hutumia ukaribu



na ushawishi wao kuzikutanisha serikali za nchi mbalimbali na serikali ya nchi tajiri pale uhusiano wa kidiplomasia unaposhindwa kutekeleza jukumu hilo.

Anaeleza kuwa inapotokea hivyo, hiyo ni fursa kubwa kwa kampuni hizo kuvuna fedha nyingi kwa muda mfupi kulingana na matukio, lakini inashauriwa kwamba isiwe utamaduni kwa serikali zinazotajwa kuona kwamba ndio mtindo wa uendeshaji wa mambo yao.

Kibamba achambua


Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia, Deus Kibamba, amesema hatua hiyo haina afya kwa taifa na inaondoa morali ya wataalamu wengi walioajiriwa katika Wizara ya Mambo ya Nje.

“Wapo wataalamu lukuki katika eneo hilo waliohitimu kikamilifu na wengine wakiwa wanaendelea kufundisha katika vyuo vikuu vya ndani, wangeweza kutumika kwenye suala hilo,” anasema Kibamba katika mahojiano na Pambazuko.

Kibamba anasema baadhi ya nchi huzitumia kampuni hizo mara chache hasa kama ina upungufu wa wataalamu katika eneo fulani, hasa kwenye taaluma adhimu, lakini hali haiko hivyo kwa Tanzania ambayo imeshajenga uwezo wa kutosha kwa wataalamu wake.

Inaendelea Uk. 8

■ Habari Kuu



Dkt. Wilbrod Slaa

Tanzania yalipa...

Inatoka Uk. 7

“Hii inaweza kueleweka kama wanahitajika wataalamu wa eneo mahsusi na baada ya kujichunguza mkabaini kuwa hamna wataalamu wa aina hiyo, ndipo mnapotafuta wataalamu kutoka nje...”

“Jambo hili linalofanyika sasa - ukiangalia msingi wake ni kutokana na yaliyotokea Oktoba 29, mwaka jana,” anaongeza.

Anasema hata kama wataalamu wa ndani hawana ufanisi wa kutosha, serikali ilitakiwa kuwakodi hao wanaoona kwamba wana weledi na ufanisi zaidi ili waje “kuwanoa” wataalamu wa ndani kwenye maeneo yenye upungufu.

Msomi asema anena

Dkt. Ismail Kamweri wa Taasisi ya Kupunguza Umasikini (TPRI) anasema Tanzania inafanya vyema kutumia kila mwanya kujiweka jirani na wale alioita “wakubwa.”

Amesema kutokana na “kuchafuka kwa sifa ya amani ya Tanzania,” ni sahihi kwa nchi kuwe-

ka bayana kile kilichotokea na kuweka taarifa sahihi kwa wakubwa wa dunia, ikiwamo Marekani, ni hatua nzuri na haipaswi kupingwa.

“Unajua namna ya kuwafikia wakubwa wa dunia kuna njia nyingi, lakini kubwa zaidi ni kutumia wazoefu wa kuunganisha makutano nao, vinginevyo wanaweza kuwa na taarifa mbaya tu za kutoka upande wa wanasiasa na wanaharakati na kuziamini, sasa kuwafikia kuna gharama zake,” ameingiza Dkt. Kamweri.

Dkt. Slaa ashangazwa

Mwanadiplomasia na mwanasiasa mkongwe nchini, Dkt. Wilbrod Slaa, ameeleza kushangazwa na kiasi hicho kikubwa cha fedha kupelekwa kwa kampuni binafsi kufanya kile alichokiita “kujisafisha” kwa serikali dhidi ya madhila wanayopitia wananchi wake.

Dkt. Slaa amesema kuwa kokote duniani, serikali yoyote inapokosea dhidi ya wananchi wake, inawajibika au kuwajibishwa na siyo suala la kuhangaika kutafuta kujisafisha kwa kutumia gharama kubwa ambayo hata hivyo haiwezi kuwa na matokeo mazuri.

“Hizi ni juhudi za kutaka kuficha jambo, lakini siku zote ukweli haufikiwi wala haufichwi, maana kama lingekuwa suala la kidiplomasia wanadiplomasia wangepanya kazi yao, lakini kwa kuwa hili ni zaidi, ndiyo sababu kuna mahangaiko ya kukodi kampuni za nje kutaka kuzitumia kujisafisha,” amesema.

Amesema juhudi hizo ni kupoteza fedha za umma pasipo sababu ya msingi kwa kuwa hata Serikali ya Marekani haiwezi kukubali kufichwa kwa uovu kwa kutumia kampuni hizo za ushawishi.

Kenya nayo yajisogeza

Pambazuko pia limeona Kenya katika jalada la FARA lenye namba ya usajili 7545, Agosti 6, 2025 kwamba ilisaini mkataba wa ushawishi wa dola za Marekani 175,000 (zaidi ya shilingi 455 milioni) kwa mwezi kwa kipindi cha miezi 12 (hivyo kutumia zaidi ya Shilingi bilioni 5.4) kabla ya mazungumzo ya Rais William Ruto na Rais Trump katika Ikulu ya White House.

Inaendelea Uk. 9

Habari Kuu ■

Tanzania yalipa...

Inatoka Uk. 8

Nigeria haijabaki nyuma

Nigeria nayo pia ilisaini mkataba wenye thamani ya dola milioni tisa kwa mwaka na DCI Group, kampuni yenye uhusiano na baadhi ya watu wa ndani wa kampuni za Rais Trump.

DCI ni kampuni ya ushauri wa masuala ya umma inayotoa huduma kamili, inayobobea katika mawasiliano na huduma za ushauri wa kimkakati kwa zaidi ya miaka 25.

Rwanda nayo haijapoa

Pambazuko limeona sehemu ya mkataba wa Rwanda na Kampuni ya Yorktown Solutions kama kampuni iliyosajiliwa kwa ajili ya kufanya shughuli za ushawishi, huku Rwanda Development Board (RDB) ikiwa ndiyo mhusika wa kigeni anayewakilishwa. Hii ilikuwa Machi 31, 2025



Rais Donald Trump

Rwanda inatajwa kulipa dola 80,000 kwa mwezi (zaidi ya shilingi bilioni 2.4) kwa mwaka - kwa washawishi huko Marekani.

Morocco hawana mchezo

Taarifa zilizopo chumba cha habari cha Pambazuko zinaonyesha kuwa Morocco ilitumia kiasi cha dola milioni 3.49 (zaidi ya Shilingi bilioni 8.8) kwa shughuli za ushawishi nchini Marekani mwaka 2025, ikitafuta kuendelea kupata uungwaji mkono na Marekani kwa msimamo wake kuhusu Sahara Magharibi.

Somalia wajikongoja

Somalia tayari imesaini makubaliano ya dola 600,000 (zaidi ya Shilingi bilioni 1.5) na BGR Group ili kufanya ushawishi na Marekani ili kuitambua Somaliland kama nchi huru.

Angola wanang'ana

Angola imethibitika kulipa dola 312,500 (zaidi ya Shilingi 812.5 milioni) kwa mwezi kwa kampuni yenye uhusiano na maofisa wa zamani wa Trump ili kuutambulisha zaidi Ushoroba wa Lobito, njia muhimu ya kusafirisha madini kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Msumbiji haitaki mchezo

Kampuni ya Brownstein Hyatt Farber Schreck iliingia mkataba na Msumbiji ili kuwakilisha kwenye ushawishi kwa Marekani.

Iliingia mkataba na kampuni hiyo na kuilipa dola za Marekani 40,000 (zaidi ya Shilingi milioni 104) kwa mwezi kwa kipindi cha miezi 12, hivyo, thamani ya mkataba huo kwa mwaka kufikia dola 480,000 (zaidi ya shilingi bilioni 2.2).

Uganda nayo imo

Julai 9, 2026, kampuni ya Skyline Capitol iliwasilisha marekebisho ya kimfumo kuongeza Ubalozi wa Jamhuri ya Uganda kuwa mhusika wa kigeni, ikiwa na jukumu la kuishauri Serikali ya Uganda kupitia ubalozi wake kuhusu mawasiliano na watunga sera nchini Marekani. Gharama zake hazikuweza kutambulika haraka kwa Pambazuko.

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA



Ujumbe wa viongozi wa dini, wakim-fariji Rais Samia Suluhu Hassan kwa maombi kufuatia kifo cha mume wake, Hafidh Ameir Hassan. Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar juzi. (Picha na Ikulu).

Serikali haina na wala haiendi eda

PAMOJA na kwamba nimeshawasilisha salaam zangu za pole kwa mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na familia yake kutokana na msiba walioupata, napenda kwa mara nyingine kuwatakiya faraja na subra wakati wote wa msiba.

Ninakujua kufiwa na mwenza na kwa hili sina masikhara. Tunayaonja mauti kwa kufa na kufiwa.

Kuna mjadala unaendelea kuhusu Mheshimiwa Rais (Mjane) kwenda eda au la? Wanashe-ria wamesema na viongozi wa dini wamesema pia. Mimi niliye kiboko wa Wajaluo, natafakari mjadala huu kwa tahadhari.

Nijuavyo na kuamini; Rais anaweza kwenda eda lakini serikali haina na haiendi eda.

Serikali yetu si mume au mke wa mtu yeyote. Kwa hiyo haiwezi kufiwa. Haina dini kwa hiyo haiwezi kwenda Eda.

Viongozi wa serikali wanaweza kuwa na wenza na kuwa na dini, lakini ni zao siyo za serikali. Wenza wa viongozi wa serikali siyo wenza wa serikali kwa sababu serikali haioi wala kuolewa.

Tusijifanye Wajaluo kwa kuchanganya katiba ya nchi na misahafu yetu ya dini. Misahafu inatufanya kuiheshimu katiba; siyo katiba inayofufanya tuiquate misahafu.

Duniani humu kuna dini zinafundisha kuwa mume akifa anazikwa pamoja na mkewe akiwa hai. Je, mkewe akiwa ni rais wa nchi akafiwa na mmewe itakuwaje?

Kuna dini ya Wajaluo inayoruhusu mume kumtandika mkewe hadharani. Je, tutavumilia kumwona rais wetu aliyeolewa na Mjaluo akitandikwa hadharani kwa mujibu wa dini ya Kijaluo? Serikali kutokuwa na dini ni salama yetu wote.

Huku kwetu misiba huwa ni jukwaa la kumaliza migogoro katika ukoo na familia. Ni wakati wa kusikilizana na kusameheana. Si mnajua msibani kila mtu ni mwigizaji halisi?!

Tuigize maridhiano ya kweli basi!

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.

Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA



Kona ya Dkt. Bisimba

Demokrasia ina maana gani kwa Watanzania?

KESHO Septemba 15 dunia itaadhimisha Siku ya Kimataifa ya Demokrasia kama ilivyopitishwa na Umoja wa Mataifa mwaka 2007.

Siku hii huadhimishwa kila mwaka, lakini kuna maswali mengi kuhusu manufaa ya kuiweka siku hii.

Je, imetusaidia kujenga taifa kidemokrasia? Tujiulize iwapo demokrasia ni ya wananchi ni kwa kiwango gani wananchi wenyewe wanashiriki katika kuijenga, kuilinda na kuidai?

Hivi tunatafakari tunachotaka ndani ya maisha ya kila siku ya Mtanzania yatokanayo na demokrasia?

Unaweza kuyajibu maswali haya kwa kuangalia hali halisi ya Tanzania kwa kutumia matukio mbalimbali likiwemo majeraha yaliyotokana na Uchanguzi Mkuu wa mwaka 2025. Majeraha ambayo hayajatibiwa na kupona.

Taarifa na tuhuma nzito kuhusu yaliyotokea katika uchaguzi ule zikiwemo vurugu, vifo na hata vizuizi kwa baadhi ya vyama vya siasa kushiriki uchaguzi ni masuala yaliyo katika mijadala hadi sasa.

Taarifa iliyotolewa na Shirika la Human Rights Watch inabainisha kuwa vurugu za kipindi cha uchaguzi huo zilisababisha vifo vya watu wengi na Tume iliyoundwa na Rais kuchunguza vurugu hizo ilitoa taarifa kuwa vilitokea vifo 518 katika mikoa 11 nchini.

Tunapoadhimisha Siku ya Demokrasia Duniani hatuwezi kabisa kuacha kuyaangalia mambo haya yaliyotokea katika tukio muhimu la kidemokrasia.

Tusidhani masuala haya yanaweza kufunikwa na tuweze kuendelea kama vile hayakutokea au yalikuwa ni ndoto tú.

Maswali yote haya yanadhihirika tukiangalia mijadala iliyoendelea wiki zilizopita mmoja ukiongozwa na Chama cha Mawakili Tanganyika na ule wa Jukwaa la Demokrasia Tanzania (TCD).

Mijadala hiyo inatulelekeza kwenye mazungumzo, mageuzi ya kisiasa na umuhimu wa kuimarisha taasisi za kidemokrasia, kama njia ya kutibu majeraha hayo.

Tumesikia sauti za wadau wakiwemo watu wanaoheshimika sana nchini wakihimiza kuondokana na lawama na kutafuta njia mahsusi za kuzuia hali iliy-



otokea mwaka uliopita.

Lakini hata katika midahalo hiyo bado kuna ombwe kwa vile suala zima la demokrasia tuitakayo hali-jaonekana kwa uwazi.

Siku moja ya kupiga kura na baada ya hapo wananchi wanabaki kuwa watazamaji kwa miaka mitano baadaye hiyo haiwezi kusemekana kuwa ni demokrasia.

Ukweli wa demokrasia ni pale kunapokuwepo na uhuru wa kutoa maoni, uhuru wakujumlahi, uwezo wakuandaa mikutano na hata maandamano ya amani, uhuru wa vyombo vya habari na asasi za kiraia kuhoji na kufuatilia masuala ya kisera na hata kishe-ria huku zikiwakumbusha wenye mamlaka wajibu wao bila hofu yoyote.

Demokrasia itoe nafasi ya kutokukubaliana. Mpinzani kisiasa asionekane adui, mwanaharakati asipewe jina baya, mwananchi muuliza maswali asionekane mkosaji.

Ujenzi wa demokrasia ni pamoja na ujenzi wa taasisi za kuilinda hiyo demokrasia. Katika siku hii mijadala wa kijasiri upite kuhusu uhuru na uadilifu wa taasisi za uchaguzi, nafasi ya Katiba na ukuu wake, uhuru wa Mahakama, nguvu ya Bunge katika kuisimamia serikali, mazingira ya ushiriki wa wananchi katika masuala yanayowahusu bila hofu.

Inabidi katika haya maadhimisho tafakari ya kina ifanyike kuangalia kama yapo tunayofanya vizuri, tuone tumekosea wapi na tuangalie umuhimu na utayari wa kujifunza kutokana na yaliyotokea.

Demokrasia isiwe ni kwa ajili ya kushinda chaguzi tu bali ihusu ujenzi wa taifa ambapo kila mwananchi ataweza kujiona ni sehemu ya taifa hili, hapo tutakuwa tunaiendea demokrasia ya kweli.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.

■ Habari

Nchimbi asubiri ‘vumbi litue,’ yuko salama



Dkt. Nchimbi

Na Waandishi WETU

NI siku 19 sasa tangu aliyekuwa Makamu wa Rais, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi ajiuzulu wadhifa wake Agosti 25, 2026, huku wasiwasi ukitanda kuhusu alipo.

Ukimya wake na kutoonekana popote, kumezua maswali lukuki ambayo hayakuwa yamepata majibu, lakini sasa Pambazuko, pasinashaka, linaweza kueleza kwamba “Dkt. Emmanuel John Nchimbi, yuko salama.”

Gazeti la Pambazuko kutoka vyanzo vinavyomfikia na kuzungumza na Dkt. Nchimbi vimehakikisha kwamba mwanasiasa huyo aliyepata kuwa kiongozi wa juu kabisa, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan yuko Dar es Salaam.

“Nchimbi yuko nyumbani kwake hapahapa Dar es Salaam, anapata muda wa kupumzika kwa sasa, anajipa muda pia wa kutafakari zaidi wakati akisubiri vumbi la sasa lipoe kidogo na mtamsikia na kumuona,” kilieleza chanzo hicho.

Watanzania waliingiwa wasiwasi baada ya kuwepo taarifa zilizoshindwa kuthibitisha aliko kiongozi huyo baada ya kujiuzulu.

Kupitia mitandao ya kijamii, mazungumzo

ya wazi, mijadala ya wasomi, wana harakati na hata vijiweni, swali kuhusu alipo Dkt. Nchimbi halikuweza kupata majibu.

Hali hiyo pia ilikolezwa na kutopatikana kwa mwanasiasa huyo na balozi baada ya simu yake ya mkononi kutopatikana pia.

Pambazuko, kwa wiki tatu sasa limekuwa katika msako wa ukweli wa wapi alipo Dkt. Nchimbi, anafanya nini, kwa nini haonekani maeneo ya wazi hata kwenye nyumba za ibada, jambo ambalo siyo la kawaida kwake.

Kupitia vyanzo vyake ambavyo vinahifadhiwa kwa sababu maalum – angalau kwa sasa, Pambazuko limebaini kuwa kiongozi huyo amejipa muda kujipumzisha.

“Nawahakikishia kiongozi (Dkt. Nchimbi) ni mzima, yupo sehemu salama, amepumzika anasubiri ‘vumbi’ litulie, atakuja mtamuona tu. Watanzania wasiwe na hofu juu ya kiongozi wao, yuko salama...”

Dkt. Nchimbi amekaa madarakani chini ya miezi kumi, baada ya kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa Rais Samia Suluhu Hassan, Agosti 27, 2025, na kuapishwa Novemba 3, 2025, akichukua nafasi ya Dkt. Philip Mpango.

Mara ya mwisho Dkt. Nchimbi kuonekana hadharani ilikuwa Agosti 22, 2026 kwenye ufun-guzi wa mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (JNHP) wilayani Rufiji, Pwani.

Hata hivyo, kwenye shughuli hiyo, kiongozi huyo alifanyakazi ya kumkaribisha rais tu, licha kwamba alipewa dakika 10 za kuzungumza. Badala yake alitumia chini ya dakika moja, akimkaribisha Rais Samia akiwa ndiye mgeni rasmi wa shughuli hiyo.

Mawasiliano mengine ya Dkt. Nchimbi na Watanzania ni Agosti 25, 2026 kupitia akaunti yake ya Instagram ambako alipitisha barua yake fupi ya kutangaza kujiuzulu kwake nafasi ya makamu wa rais na siku iliyofuata Agosti 26, 2026, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kikamfuitia uanachama wake.

Profesa Saffari asifu sheria kuandikwa Kiswahili

Na Waandishi WETU

NGULI wa sheria nchini, Profesa Abdallah Saffari amesifu hatua ya serikali kukubali kuandika sheria zote kwa Kiswahili, akisema kuwa ni moja ya mapinduzi makubwa ya mfumo wa haki nchini.

Mbali na hilo, ameshauri Tanzania iwe na mahakama ya juu zaidi – ya upeo (supreme court) badala ya mashauri kuishia kwenye ngazi ya mahakama ya rufani pekee.

Akizungumza na Pambazuko mwishoni mwa wiki, Profesa Saffari amesema mahakama ya upeo inatoa haki zaidi, kwani mtu akitiwa hatiani katika mahakama za chini ana uwezo wa kuendelea kutafuta haki yake mpaka kwenye mahakama hiyo.

“Tanzania ni pekee Afrika ambayo haina supreme court (mahakama ya upeo), nafikiri ni serikali kuamua suala hilo muhimu linaloongeza wigo wa utoaji haki nchini,” amesema Profesa Saffari.

Kuhusu umuhimu wa matumizi ya Kiswahili katika sheria za Tanzania, amesema yeye ni miongoni mwa wajumbe wa kikosi kilichofanya kazi za kubadilisha sheria kutoka kwenye Kiingereza kwenda Kiswahili na kwamba huenda mwakani kazi hiyo itakuwa imekamiliwa rasmi.

Profesa Saffari ambaye ni mtaalam na mtunzi wa vitabu vya Kiswahili, amesema moja ya maandiko yake ya kisheria aliwahi kushauri Kiswahili kitumike rasmi kuwa lugha ya mahakama, jambo ambalo anasema linakwenda kutimia hivi karibuni.

Amesema ndoto yake ni kuona wigo wa haki unaongezeka na kwamba matumizi ya Kiswahili yatafanya wengi kufuatilia na kuelewa mwenendo mzima wa haki.



Mwanasheria nguli na mtunzi wa vitabu, Profesa Abdallah Saffari, akizungumza katika mahojiano maalum na mhariri wa habari wa gazeti hili, Arodia Peter ofisini kwake jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. (Picha na Mpigapicha Wetu).

Baadhi ya vitabu vyake vinaendelea kutumiwa kwenye shule za sekondari, sheria na vyuo vikuu mbalimbali hususani kwenye rejea ya fasihi. Vitabu hivyo ni pamoja na harusi, joka la mdimu, mashtaka ya jinai na utetezi na vingine kikiwamo haja ya kuwa na tume huru ya Taifa ya uchaguzi Tanzania alichokiandika mwaka 2010.

Aidha, Profesa Saffari ameshauri matumizi ya Kiswahili yawekwe rasmi kwenye Katiba ya nchi kama walivyofanya Kenya ingawa kwao siyo lugha rasmi inayotumika kila mahali kama ilivyo Tanzania.

“Kwa nini Kenya inaonekana wako mbele kwenye Kiswahili wakati wao vyombo vya habari zikiwamo televisheni, karibu vyote, bungeni na kila mahali wanatumia Kiingereza, ingawa kisheria kwa maana ya Katiba yao inaonyesha Kiswahili kimetambuliwa rasmi.

“Kuna mtu mmoja amewahi kuniuliza swali kwamba kati ya sheria na Kiswahili unapenda zaidi nini, sikusita, nilimjibu moja kwa moja mimi napenda sana lugha ya Kiswahili, ninapokaa na magwiji tunafanya uchambuzi wa hili na lile kuhusu Kiswahili, naona raha sana na nikiwa na magwiji kama akina Andanenga, watunzi wa mashairi, mimi najifunza zaidi na kupata mambo ya ziada kuhusu lugha hiyo adhimu,” amesema.

■ Habari

JKT wapya ‘kujinoa’ kwa usafi Dar



Mkuu wa Wilaya Ilala, Edward Mpogolo, akishirikiana na baadhi ya viongozi wa wilaya hiyo kufanya usafi wa kuondoa taka eneo la Kariakoo baada ya kuzindua kampeni endelevu ya kufanya usafi kila Jumamosi katika Jiji la Dar es Salaam juzi. (Picha na Mpigapicha Wetu).

Na Hellen NGOROMERA

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ametangaza kuwatumia vijana waliomaliza mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) katika kampeni ya kuimarisha usafi mkoani humo.

Akizungumza mwishoni mwa wiki siku chache tu baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuonyesha kukerwa na kukithiri kwa uchafu katika jiji hilo kuu la kibiashara nchini, Chalamila alisema vijana hao watatumika kusimamia na kuwadhibiti watu wanaotuma takataka hovyoo.

Chalamila ameeleza hayo wakati akiainisha mikakati ya kushughulikia karipio alilolitoa Rais Samia kuhusu kukithiri kwa uchafu katika Jiji la Dar es Salaam na miji mingine mikubwa nchini.

Kwa upande wake, Chalamila amewaelekeza wakuu wa wilaya wote mkoani mwake kuandaa utaratibu wa kuwatumia vijana hao waliomaliza JKT kufanya shughuli hiyo.

“Nimewaeleza ma-DC kutafuta utaratibu wa haraka ili kuwawezesha vijana hao wawe wadau wakubwa wa usimamiaji wa sheria za utupaji wa taka ovyo,” amesema Chalamila.

Chalamila amesema vijana hao wa JKT watapewa rungu la kukamata watupa taka katika kila kata ya jiji analoliongoza baada ya kukamilika kwa zoezi la upatikanaji wake.

“Utaratibu huo utawekwa vizuri na mkoa na utatangaza vijana watachaguliwa kusimamia zoezi hilo ikiwemo kuwatoza faini wakiukaji wa jambo hilo,” alifafanua.

Pamoja na mambo mengine, mkuu huyo wa mkoa amemtaka kila mwananchi kwenye eneo lake kuhakikisha ana chombo maalumu cha kuhifadhi takataka, lakini pia kila mwenye gari ahakikishe ana chombo cha kutupia takataka ndani ya gari lake.

“Kila mmoja akatae kutupa taka kila mahali kwa sababu mzalishaji mkubwa wa taka ni mwananchi mwenyewe, tukienda kwa elimu hiyo ninaamini tutavuka na kila mmoja atao-na fahari kukaa kwenye ardhi yetu ikiwa safi na salama,” amesema Chalamila.

Katika karipio lake alilolitoa Septemba 2, mwaka huu, Rais Samia alieleza kukasirishwa na kukemea vikali hali duni ya usafi katika Jiji la Dar es Salaam na miji mingine mikubwa nchini.

Rais Samia ambaye alieleza hayo wakati wa hafla ya kuwaapisha wakuu wa mikoa na makatibu tawala katika Ikulu Ndogo ya Tunguu, Zanzibar alieleza kutofurahishwa na mwonekano wa Jiji la Dar es Salaam akieleza namna maeneo mbalimbali ya jiji hilo hasa mitaani kulivyo kuchafu hali inayoshusha hadhi ya jiji hilo.

Aligusia pia kuhusu upendeleo wa zabuni za usafi akilaumu mifumo ya baadhi ya hal-mashauri kutoa zabuni za usafi kwa madiwani kama njia ya ‘kukaa nao vizuri’ wakati madiwani hao hawana uwezo wa kifedha wala vifaa vya kusimamia usafi. Aliagiza zabuni hizo zipewe wakandarasi wenye uwezo mkubwa wa kazi

Kutokana na kauli hiyo ya rais, RC Chalamila pamoja na wakuu wa wilaya na madiwani walianza kufanya vikao vya mikakati na kampeni kubwa za usafi wa mazingira kila Jumamosi katika maeneo mbalimbali ya jiji ili kuondoa aibu hiyo.

Msomi ataka takwimu kukua uchumi ziguse jamii

Na Waandishi WETU

MHADHIRI wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Idara ya Sanaa Bunifu, Dkt. Dominicus Makukula, amesema wakati umefika kwa wataalamu kueleza sababu za kukua kwa uchumi wa nchi, wakati Watanzania wengi bado wako kwenye lindi la umasikini.

Amehoji kuwa wakati takwimu zinazotolewa kila wakati na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi zikionyesha kuwa uchumi wa Tanzania unakua, iweje watu wake waendeleo kuwa masikini.

Akizungumza na Pambazuko katika mahojiano maalum, Dkt. Makukula, amesema utafiti unaofanywa kuhusu ukuaji wa uchumi wa Tanzania unapaswa kueleza sababu na njia za kukomesha umasikini unaoonekana wazi.

Dkt. Makukula ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Baraza la Utumishi wa Kitaalum la UDSM (Udasa), ameshauri pia kuwa ukuaji wa uchumi katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma kusichukuliwe kuwa kielelezo cha uchumi wa nchi nzima kukua.

Msomi huyo amesema kuna aina fulani ya shughuli zinazofanyika katika maeneo hayo na hivyo kuyafanya kuwa kielelezo, kunashindwa kuonyesha ukweli kuhusu hali ya umasikini ambao umekithiri mikoa mingi ya pembezoni.

Dkt. Makukula amesema miaka michache iliyopita takwimu hizo zilionyesha kuwa Tanzania imeingia kwenye uchumi wa kati wa juu, lakini baadaye ikarekebishwa kuonyesha kuwa ni uchumi wa kati wa chini, jambo ambalo limezidi kuwachanganya wananchi.

“Tunapaswa kuwa tunaona huo utafiti. Matokeo ya utafiti yawafikie watu waweze kuona thamani ya kuwajibika kwao na kupima namna wanavhochangia ukuaji wa uchumi wao,” amesema.

Anabainisha kuwa ukifuatilia hali ya Dar es Salaam utabaini kuwa baadhi ya watu wana uchumi mzuri sana na wakati huohuo, wapo wenye uchumi mbaya zaidi. “Wakati wewe unahangaika kutafuta shilingi hamsini, kuna jamaa jirani yako anaporomosha ghorofa la vyumba 30 hadi, mpaka unachoka, wengine

wanabadilisha magari, lakini wewe huna hata baiske-li,” anasema.

Mhadhiri huyo anasema mambo hayo ni lazima yaangaliwe na kuzingatiwa katika utafiti ili majibu yashabihi hali halisi ya maisha ambayo Watanzania wengi wanaishi. “Hivyo vitu lazima viangaliwe, ninamini kukua kwa uchumi wa nchi ni sawasawa na baba katika familia yake. Kama zamani kipato chake kilikuwa Shilingi 150,000, uchumi ukikua anapaswa kupata chakula kizuri mwezi mzima...”

“Baba ambaye mtoto wake walikuwa anatembea bila viatu, sasa aweze kumudu kununua jozi tatu au nne za viatu. Kama mke alikuwa anavaa malapulapu, aanze kuvaa nguo nzuri, hiyo ndiyo tafsiri ya kukua kwa uchumi,” anasema msomi huyo.

Soko la ajira nchini

Dkt. Makukula amezungumzia ubora wa elimu katika ukanda wa Afrika Mashariki na duniani kwa ujumla, ambapo amesema taasisi za elimu zinapaswa kuwa na mitaala ambayo inaendana na matakwa ya soko la ajira.

Amesema UDSM kila wanapotaka kuandaa mitaala mipya, lazima washirikishe wadau katika sekta husika, akieleza kuwa Shule Kuu ya Biashara ambao wamekuwa wakishirikisha wadau mbalimbali kutoka sekta ya mabenki kwenda kutoa ushauri wa wataalam wanaowahitaji. Katika mahojiano hayo, Katibu huyo wa Udasa amesifu mabadiliko makubwa katika kuandaa mitaala ya elimu ya vyuo vikuu yaliyofanywa na serikali ya China hivi karibuni.

Amesema serikali ya nchi hiyo imefuta program za shahada ya kwanza zaidi ya 1,200 na kuleta kozi ambazo zinaendana na masuala ya ubunifu katika sayansi kwa kuangalia nafasi yao, mahitaji na ushindani walionao duniani.

“Wachina kuna baadhi ya mambo mazito wamey-aondoa kwenye shahada na sijui wameyapeleka wapi. Kwa mfano degree (shahada) ya sanaa wameiondoa, na nyingine zinazohusiana na masuala ya sayansi ya jamii, nyingi wamezifuta. Wenzetu Wachina wameangalia mahitaji na mabadiliko ya kielimu na ushindani wa kidunia” amesema Dkt. Makukula.

Habari

DSE yavunja rekodi, mtaji wafika trilioni 40/-



Mkurugenzi Mtendaji wa DSE, Peter Nalitlela

Na Costantine MUGANYIZI

SOKO la Hisa la Dar es Salaam (DSE) limeandika historia kubwa kwa kufikia kiwango cha juu cha mtaji cha Shilingi trilioni 40.

Hatua hiyo inadhihirisha kuongezeka kwa thamani ya kampuni zilizoorodheshwa na imani ya wawekezaji katika soko la mitaji nchini.

Thamani ya jumla ya kampuni zote zilizoorodheshwa DSE ilifikia rekodi ya Shilingi trilioni 40.3 mnamo Septemba 10, 2026, ikilinganishwa na Shilingi trilioni 38.74, kilichokuwa kiwango cha juu kilichorekodiwa Agosti 28 mwaka huu.

Hii ina maana kuwa ndani ya kipindi kisi-chozidi wiki mbili, thamani ya soko imeongezeka kwa takribani Shilingi trilioni 1.56, sawa na ongezeko la karibu asilimia nne.

Kwa mtazamo mpana zaidi, thamani ya soko imeongezeka kwa kasi kubwa katika kipindi cha mwaka mmoja.

Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa mnamo Septemba 10, 2025, mtaji wa jumla wa DSE ulikuwa Shilingi trilioni 21.73, ikimaanisha kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja, soko hilo lilishuhudia ongezeko la takribani Shilingi trilioni 18.57, sawa na asilimia 85.5.

Wataalamu wa soko la mitaji wanasema kuvuka kwa kiwango hicho kunaashiria kukua kwa nafasi ya DSE katika uchumi wa Tanzania, hasa katika kuchochea upatikanaji wa mitaji ya muda mrefu kwa kampuni na kutoa fursa zaidi kwa wawekezaji kushiriki katika ukuaji wa biashara. Hatua hiyo pia inakuja wakati Tanzania inaanza kutekeleza Dira ya Maendeleo ya 2050, ambayo inaweka sekta binafsi katika nafasi muhimu katika kufadhili mabadiliko ya kiuchumi yanayolenga kuifanya nchi kuwa na uchumi wa thamani ya dola trilioni moja.

NMB yainua kiwango cha soko

Miongoni mwa kampuni zilizochangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa thamani ya DSE ni Benki ya NMB, ambayo sasa imeingia katika kundi jipya la kampuni zenye thamani ya zaidi ya Shilingi trilioni 10.

NMB ilikuwa kampuni ya kwanza iliyoorodheshwa DSE kuvuka kiwango hicho baada ya bei ya hisa zake kufikia Shilingi 2,130 mnamo Agosti 28 mwaka huu na kuipa benki hiyo mtaji wa soko wa takribani Shilingi trilioni 10.65.

Mkurugenzi Mtendaji wa DSE, Peter Nalitlela, amesema mwenendo huo unaonyesha kuimarika kwa imani ya wawekezaji kwa kampuni zilizoorodheshwa nchini na kuvutia zaidi kwa soko la Tanzania. Kwa mujibu wa Nalitlela, ongezeko kubwa la thamani ya NMB baada ya mgawanyo wa hisa kwa uwiano wa 1:10 limekuwa miongoni mwa vichocheo muhimu vya kupanda kwa thamani ya jumla ya DSE.

Habari ■

DSE yavunja rekodi...

Inatoka Uk. 16

Kabla ya mgawanyo huo, thamani ya soko la NMB ilikuwa takribani Shilingi trilioni 8.85, lakini ilipanda hadi Shilingi trilioni 10.65 trilioni ndani ya wiki moja baada ya hatua hiyo.

“NMB imekuwa kampuni ya pili yenye thamani kubwa zaidi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), baada ya Safaricom ya Kenya, na kuwa benki ya kwanza katika EAC kufikia thamani ya takribani dola za Marekani bilioni 3.84,” alisema Nalitolela.

Mtaalamu wa masoko ya mitaji, Godfrey Kamugisha, amesema mafanikio ya NMB pamoja na rekodi mpya ya DSE yanaonyesha kuongezeka kwa imani ya wawekezaji kwa kampuni hiyo na mazingira ya uwekezaji nchini.

Amesema mafanikio ya NMB yanaweza pia kuhamasisha kampuni nyingine kubwa za Tanzania kuingia DSE kwa kuuza hisa kwa umma.

Kwa mtazamo wake, kuongezeka kwa idadi na ukubwa wa kampuni zilizoorodheshwa kutasaidia kuongeza kina cha soko na kutoa chaguo pana zaidi kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa.

Mtaji wa ndani nao wakua

Wakati mtaji wa jumla wa soko umevuka Shilingi trilioni 40, mtaji wa kampuni za ndani pekee umefikia rekodi ya Shilingi trilioni 28.1.

Hii inaonyesha kuongezeka kwa thamani ya kampuni za Kitanzania zilizoorodheshwa na uwezo unaokua wa DSE kukusanya mitaji kutoka kwa wawekezaji kwa ajili ya biashara za ndani.

Kwa kampuni zinazotafuta fedha kwa ajili ya upanuzi, kuimarisha mitambo, kuongeza uzalishaji au kuingia katika masoko mapya, soko la hisa linaweza kutoa chanzo cha mtaji wa muda mrefu bila kutegemea mikopo ya benki pekee.

Kwa wawekezaji, kwa upande mwingine, ukuaji wa thamani ya kampuni zilizoorodheshwa unaongeza fursa za kumiliki sehemu ya biashara na kunufaika na ukuaji wake kupitia ongezeko la bei za hisa na gawio.

Kasi ya ukuaji wa DSE inaonekana wazi katika rekodi zilizowekwa katika kipindi cha mwaka mmoja.

Septemba 10, 2025, mtaji wa jumla wa soko ulikuwa Shilingi trilioni 21.73. Agosti 28, 2026, ulifikia Shilingi trilioni 38.74, kabla ya kuvuka rasmi kiwango cha shilingi trilioni 40 na kufikia Shilingi trilioni 40.3 Septemba 10, mwaka huu.

Kwa jumla, soko limeongeza takribani Shilingi trilioni 18.57 ndani ya mwaka mmoja.

Dira 2050 yaweka mazingira mapya

Rekodi hiyo imepatikana wakati Tanzania ikiingia katika utekelezaji wa Dira 2050, ambayo ilianza rasmi Julai 1, 2026.

Tanzania inalenga kujenga uchumi wa kufikia thamani ya dola trilioni moja, huku sekta binafsi ikitarajiwa kutoa takribani asilimia 70 ya fedha zitakazohitajika katika utekelezaji wa mabadiliko hayo.

Katika mazingira hayo, soko la mitaji linaweza kuwa moja ya nyenzo muhimu za kufanikisha malengo hayo.

Soko lenye kampuni nyingi, kubwa na zenye ukwasi linaweza kusaidia kuunganisha mitaji ya wananchi, mifuko ya pensheni, taasisi za uwekezaji na wawekezaji wa kimataifa na mahitaji ya mitaji ya kampuni zinazopanua biashara.

Hivyo, kuvuka kwa DSE ukuaji huu si rekodi ya takwimu pekee bali ni ishara kwamba soko la mitaji linaanza kuchukua nafasi kubwa zaidi katika uchumi wa Tanzania, wakati nchi ikitafuta kuongeza uwekezaji binafsi na kupunguza utegemezi wa vyanzo vya kawaida vya fedha.





Uchumi & Biashara

Madhara kupanda mfumko wa bei 'yatokota'



Na Mwandishi WETU

WACHUMI wanaonya kuwa ingawa takwimu zinaonyesha kuwa mfumko wa bei haujafika kwenye hali mbaya sana, lakini mwenendo wake katika miaka ya hivi karibuni ni suala linalopaswa kuanza kufikiriwa kwa kina na hatua kuchukuliwa.

Takwimu zinazotolewa na Benki Kuu (BoT) zinaonyesha kuwa mfumko wa bei nchini Tanzania umeendelea kubaki ndani ya lengo la kitaifa na vigezo vya kikanda vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na SADC.

Lakini kiwango cha mfumko wa bei kimekuwa kikipanda kila takwimu mpya zinapotolewa.

Mathalan, ripoti ya hali ya uchumi (MER) iliyotolewa hivi karibuni na BoT inaonyesha kuwa mfumko wa bei wa mwaka hadi mwaka ulifikia asilimia 4.2 mwezi Julai 2026, ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwezi Juni 2026 na asilimia 3.3 mwezi Julai 2025.

“Pamoja na kwamba kiwango hiki hakijafikia viwango vya juu vya kurekodiwa au vile vya ukomo wa kikanda, mwenendo huu wa kupanda kwa mfumko wa bei kwa miezi ya hivi karibuni unaonyesha wazi presha inaongezeka katika uchumi wa watu binafsi,” anabainisha

mchumi mmoja aliyezungumza na Pambazuko.

Taasisi za uchumi ikiwemo BoT zinataja athari za gharama za mafuta ambazo zimesababisha kupanda kwa gharama za usafirishaji kuwa ndio kisababishi kikubwa kwa ongezeko hili la mfumko wa bei.

Kwa mujibu wa MER hiyo, mfumko wa bei wa msingi (core inflation) - ambao hauhusishi chakula na nishati, ulipanda hadi asilimia 3.9 mwezi Julai 2026 kutoka asilimia 3.7 mwezi Juni na asilimia 1.9 mwezi Julai 2025.

Vilevile, mfumko wa bei za nishati, mafuta, na huduma uliongezeka hadi asilimia 6.9 mwezi Julai 2026.

Hata hivyo, BoT inabainisha katika ripoti hiyo kuwa utulivu wa bei za vyakula (ambazo zilibaki asilimia 4.1 mwezi Julai) kutokana na mavuno na akiba ya chakula nchini, umesaidia kwa kiasi kikubwa kuzuia mfumko wa bei usipande kwa kasi zaidi.

Athari kwa mwananchi

Kupanda huku kwa mfumko wa bei kunaamaanisha kuwa mwananchi hivi sasa analazimika kutumia kiasi kikubwa zaidi cha fedha kupata bidhaa au huduma ile ile aliyokuwa anaipata mwaka jana.

Wachumi wanabainisha kuwa hii inaamaanisha kuwa gharama za maisha zinazidi kuongezeka.

Wachumi hao wanasema pia kuwa kwa mujibu wa misingi ya kiuchumi, kupanda huku kwa mfumko wa bei kunamaanisha kupanda kwa gharama za usafiri na huduma.

“Inaamaanisha kuwa kiasi kile kile cha fedha anachopata mwananchi sasa hivi kinamnunulia bidhaa na huduma chache zaidi ikilinganishwa na mwaka uliopita,” anafafanua mchumi huyo.

Kwa kuwa gharama za usafirishaji zimepanda na athari zake zinasambaa kwenye bidhaa nyingine, kaya nyingi zitalazimika kutumia sehemu kubwa ya kipato chao kwenye mahitaji ya msingi ya kila siku, hivyo kupunguza fedha za kuweka akiba au kuwekeza.

Hata hivyo, mchumi huyo ametoa msisitiza kwa serikali kuendelea kuimarisha Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA) kwani takwimu zinaonesha kuwa utulivu wa bei za vyakula ndio umeshikilia mfumko wa bei kwa sasa.

Dhahabu bado kinara pato la kigeni

Na Mwandishi WETU

DHAHABU imeendelea kuwa mhimili wa pato la kigeni kwani mauzo yake ndiyo yanaongoza kuingizia nchi fedha za kigeni, Benki Kuu Tanzania (BoT), imeeleza.

Ripoti ya hali ya uchumi kwa mwezi Julai (MER) iliyotolewa na BoT hivi karibuni inaonyesha kuwa kwa jumla sekta ya mauzo ya nje imeendelea kuonyesha ustahimilivu na ukuaji mzuri kwa mwaka unaoishia Julai 2026.

Katika kipindi hicho, BoT inaeleza, jumla ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 16.5 na kufikia dola za Marekani milioni 19,985.8 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2025.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, dhahabu imeendelea kuwa bidhaa nambari moja na nguzo kuu nchini kwa kuingiza fedha nyingi zaidi za kigeni.

Katika mwaka unaoishia Julai 2026, mauzo ya dhahabu nje ya nchi yalipanda kwa asilimia 37.4 na kufikia dola za Marekani milioni 5,670.7 (kutoka dola milioni 4,127.1 mwaka uliopita).

Mchango wa dhahabu pekee unawakilisha asilimia 47.4 ya mapato yote ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi.

Kwa mujibu wa BoT, dhahabu imeendelea kuwa kinara wa kuingiza fedha za kigeni kutokana na bei nzuri ya madini hayo katika soko la kimataifa.

Huduma nyingine

Mapato ya Tanzania kutoka kwenye masoko ya kimataifa yanaonyesha taswira nzuri ya ukuaji wa uchumi, ikichangiwa na mchanganyiko wa sekta za huduma, uzalishaji wa viwandani, na kilimo.

Mbali na dhahabu, mapato ya fedha za kigeni yamechangiwa pia na bidhaa na huduma nyingine kadhaa ikiwemo utalii na mazao ya kilimo.

Katika sekta ya huduma, utalii unaendelea kufanya vizuri kama mhimili mkuu wa kuingiza fedha za kigeni. Kuimarika kwa sekta hii kulii-



wezesha kuingiza kiasi cha dola za Marekani milioni 4,292.8, kwa mujibu wa ripoti hiyo ya BoT.

Wakati huohuo, sekta ya usafirishaji nayo ilirekodi ukuaji wa asilimia 29.7 na kufikisha mapato ya dola za Marekani milioni 3,221.5, mafanikio yaliyotokana na kuongezeka kwa shehena ya mizigo inayopitishwa kuelekea nchi jirani (transit goods), hasa kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Kwa upande wa bidhaa za viwandani, nchi imepiga hatua kubwa kwa kushuhudia ukuaji wa uzalishaji kwa asilimia 46 na kulingizia taifa dola za Marekani milioni 2,215.5.

“Ongezeko hili lilichochoewa zaidi na mauzo ya bidhaa za chuma na nondo, vito vya kioo, pamoja na nguo,” inasema BoT katika ripoti hiyo.

Sekta ya kilimo pia haikubaki nyuma, ambapo uzalishaji wa mazao ya asili uliongezeka kwa asilimia 14.9 na kufikia thamani ya dola za Marekani milioni 1,628.8.

Ndani ya kundi hili la mazao ya asili, tumbaku ilikuwa kinara kwa kuingiza dola za Marekani milioni 588.6, ikifuatiwa na korosho zikiingiza dola za Marekani milioni 479.3, huku kahawa ikisaidiwa na bei nzuri katika soko la dunia na kuingiza dola za Marekani milioni 396.0.

■ Habari

Mjadala TCD waibua mahitaji Tanzania mpya



Makamu
Mwenyekiti CCM
Bara, Stephen
Wasira

Na Mwandishi WETU

MJADALA mzito kuhusu hatma ya Tanzania baada ya matukio ya Oktoba 29, 2025, umeibua mahitaji ya wadau kuhusu namna nchi inavyoweza kujengwa upya na kuepuka madhara yatokanayo na mwenendo wa baadhi ya wanasiasa.

Aidha, mjadala huo umeweka msisitizo kwenye ulazima wa kutafuta namna bora ya kuiweka nchi pamoja.

Katika mjadala wa kitaifa ulioandaliwa na kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) uliomalizika wiki iliyopita jijini Dar es Salaam, wadau walioshiriki walitumia fursa hiyo kushauri kuhusu yanayopaswa kufanyika kutatua changamoto zinazoikumba nchi na kuiweka Tanzania bora zaidi sasa na baadaye.

Wadau hao kutoka asasi za kiraia, vyama vya siasa, wanataaluma, wadau wa maendeleo, taasisi za serikali, wanasheria, wasomi, vijana na makundi mengine, walitumia nafasi hiyo kujiuliza na kujibu maswali kuhusu mwelekeo na mustakabali wa nchi “baada ya kupitia vipindi vigumu.”

Kwamba nini kifanyike kuhusu mwelekeo wa siasa za nchi, uhusiano baina ya vyama, dini, wanasiasa na kuangalia mustabali wa taifa, namna ya kujenga maridhiano na hatua zinazohitajika kurejesha imani miongoni mwa Watanzania kutokana na matukio ya Oktoba 29, 2025 na yaliyofuata.

Akizungumzia kuhusu mwelekeo wa taifa, waziri mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, alieleza kuwa hadi sasa umoja na mshikamano ambao ulijengwa kwa gharama kubwa na kuwekewa misingi tangu ulipopatikana uhuru wa Tanganyika unaonekana kuvurugwa na watu wachache, hivyo kushauri kurejea katika misingi ya awali.

Alisema ni jambo la kushangaza kuona sasa hivi suala la amani linachukuliwa kuwa la kulindwa kwa mtutu wa bunduki, hasa baada ya kukiukwa kwa misingi iliyowekwa awali ya amani ya kweli iliyojengwa chini ya kufutwa kwa ubaguzi wa aina zote, ikiwemo wa kidini, kiitikadi, kikanda na kikabila, suala ambalo linaonekana kupuuzwa kwa sasa.

“Amani hailindwi kwa mtutu wa bunduki... ni lazima kurudi kwenye msingi, kuwe na usawa, kusiwe na ubaguzi wa aina yoyote...”

“Hapa amani ni jambo la msingi na lazima tukubaliane, kama kuna kitu kinakuja kutisha amani yetu lazima wote tukiache. Vyama vihakikishe vinaunganisha wananchi, tusifikiri kuwa amani italetwa kwa mgawanyiko, hapana,” alisema Jaji Warioba.

Alisisitiza kuwa Tanzania inahitaji kurejea katika misingi ya usawa, uadilifu, uwajibikaji na uzalendo, huku akizitaka taasisi na vyama vya siasa kutafuta njia za kuwaunganisha wananchi.

Alisema siku hizi viongozi wakisimama wanaita mikutano ya hadhara ya wanachama wao, wanakuwa na sare yao, wa sare za vyama vingine hawasogei pale, wakisogea ni ugomvi kwa hiyo wanasiasa wamewagawa wananchi katika siasa na katika jamii, ikiwa ndio chanzo cha matatizo ya amani ya nchi.

Inaendelea Uk. 21

Mijadala TCD...

Inatoka Uk. 20

“Pia hivi sasa zimeanza jitihada za kuzua ukabila na sasa hivi tunazungumza hata mambo ya maadili tunasema machifu wasimamie maadili, tumeanza kuzungumza maadili ya makabila wakati tulikuwa tumeshajenga maadili ya kitaifa, tunarudisha ukabila kwa njia nyingine...”


“Hata kwenye masuala ya imani, sasa kuna mpasuko wa dini kwa sasa hivi na unaanza kutugawa na kuwagawa viongozi na pia ukanda umezidi, watu wanaanza kujitazama kwa msingi wa kanda. Utaifa umezuka, u-Zanzibari na u-Tanganyika, tunaanza kujiona sisi Wazanzibari sisi Watanganyika na tunadai haki zetu,” alisema.

Makamu wa kwanza wa Rais mstaafu wa Zanzibar, Othman Masoud Othman alisema baadhi ya mambo yanaendeshwa kwa mazoea na kujuana, badala ya kufuata Katiba, hali ambayo, kwa maoni yake, inaweza kuleta vurugu iwapo mtu ataamua kudai utekelezaji wa Katiba kikamilifu.

Sheikh Issa Ponda, Kiongozi wa Shura ya Maimamu, alisema kizazi cha sasa kinataka kuona Tanganyika ikiwa na nafasi yake ndani ya Muungano, akirejea hoja ya serikali tatu iliyowahi kujadiliwa na Tume ya Jaji Warioba.

Waziri wa zamani, Profesa Anna Tibaijuka, amesema utambulisho wa Tanganyika hauwezi kuondolewa kwa kuimarisha utambulisho wa Zanzibar.

Tibaijuka alisema yeye binafsi angependa kuona serikali moja, akisisitiza umuhimu wa umoja wa kitaifa.



Jaji Warioba

Makamu Mwenyekiti wa CCM, Stephen Wasira, kwa upande wake alihoji sera ya ACT Wazalendo ya “Zanzibar yenye mamlaka kamili”, akitaka kufanuliwa kama mamlaka hayo yanamaanisha Zanzibar kuwa dola yenye mamlaka kamili au bado kuwa sehemu ya Muungano.

Kwa upande mwingine, kesi ya Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu, anayekabiliwa na mashtaka ya uhaini katika Mahakama Kuu, iliibuliwa katika mkutano huo, ambapo Katibu Mkuu wa ACT Wazalendo, Ado Shaibu Ado, alisema kumuachia Lissu ni miongoni mwa hatua muhimu zinazoweza kujenga mazingira ya maridhiano.

Ado alisema ni dhahiri kuna sauti kubwa inayotaka Tanzania ifikie maridhiano, lakini akaonya kuwa maridhiano ya kweli yana masharti na misingi yake na yatafanikiwa tu kwa kumuachia Lissu, kushughulikia kesi anazodai kuwa na mwelekeo wa kisiasa, kuweka ukweli, haki na uwajibikaji mbele katika kushughulikia vifo vilivyotokea baada ya uchaguzi wa Oktoba 29, 2025,” alisema.

Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), Boniface Mwabukusi, alitoa mwito kwa CCM kusi-mamia hatua ya kufutwa kwa kesi zenye viashiria vya kisiasa, akisema hilo linaweza kuwa sehemu ya mchakato wa uponyaji wa taifa.

Mwabukusi alionya dhidi ya kukimbilia mchakato wa Katiba Mpya bila kwanza kujenga mazingira ya maelewano, akisisitiza kuwa haoni uwezekano wa kuandika Katiba Mpya kwa utulivu ikiwa taifa bado halijaweza kukubaliana kuhusu yaliyotokea.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanataaluma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Udasa), Profesa Elgidius Ichumbaki, alihoji utekelezaji wa ahadi ya CCM ya kuanzisha mchakato wa Katiba Mpya ndani ya siku 100, akiuliza kwa nini wanachama wa chama hicho wanaozungumzia suala hilo wanaonekana kukumbana na matatizo.

Ichumbaki alimtaja Dkt. Emmanuel Nchimbi kama mfano wa mwanasiasa ambaye msimamo wake wa hadharani kuhusu Katiba Mpya umehusishwa na hatua zilizochukuliwa dhidi yake ndani ya CCM. Hata hivyo, Wasira alipinga hoja hiyo, akisema si kweli kwamba mwanachama anayezungumzia mambo yanayotakiwa na wananchi “anashughulikiwa” kwa sababu hiyo, akisisitiza kuwa CCM yenyewe ndiyo imeahidi Katiba Mpya.

■ Kutoka Kesi ya Lissu

Ushahidi wa simanzi kutoka kwa Heche



Makamu Mwenyekiti wa Chadema, John Heche (katikati), akijadiliana jambo na mawakili Deogratias Mahinyila (kushoto) na Paul Kisabo, wakati wa kuwasilisha ushahidi wa utezi katika kesi ya uhaini inayomkabili mwenyekiti a chama hicho, Tundu Lissu, katika Mahakama Kuu Masijala Ndogo ya Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. (Picha na Pambazuko)

Na Mwandishi wetu

UMATI wa watu unaofuatilia ushahidi wa kesi ya uhaini katika Mahakama Kuu - Masijala Ndogo ya Dar es Salaam, umepitishwa katika ushahidi wenye mnyororo wa matukio ya simanzi uliowahi kufanywa viongozi wa chama hicho.

Mwenye kubeba simulizi zaidi ya simanzi ni kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Chadema, John Heche wakati akiendelea kutoa ushahidi wake katika kesi inayomkabili mwenyekiti wake, Tundu Lissu.

Heche, shahidi wa tano katika kesi hiyo ametumia muda mwingi kuieleza mahakama namna ambavyo vyombo vya dola vimekuwa vikiwaandama viongozi na watu wa karibu wa viongozi hao, ikiwemo madai ya kuwakamata, kuwateka, kuwafungulia kesi na hata wengine kuuawa katika mazingira ya kutatanisha.

Lissu anakabiliwa na kesi ya uhaini namba 19605/2025 iliyodumu kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa, ikiwa chini ya majaji watatu wakiongozwa na Jaji Jaji Dunstan Ndunguru. Majaji wengine ni James Karayemaha na Ferdinand Kiwonde.

Katika ushahidi wake alioanza kuutoa Septemba 9, 2026, Heche aliwaeleza majaji kuwa ameshiriki uchaguzi mara kadhaa akiwa mgombea ambapo amewahi kuwa diwani, mbunge na kushiriki kwenye kampeni za chama chake, lakini zote ziliambatana na maumivu makubwa.

Maumivu hayo ni pamoja na kutekwa, kuenguuliwa kwa wagombea kwa kuambiwa hawajui kuso ma na kuandika na kuibwa kwa fomu za viapo vya mawakala.

Heche ameipitisha mahakama katika simulizi za matukio hayo yenye simanzi akielekea kutoa ufafanuzi wa msimamo wa chama wa “No Reform No Election” ambapo alieleza kuwa ilimaanisha kuweka msukumo kwenye mabadiliko ya kimfumo hasa katika kusimamia uchaguzi huru na wa haki, kuanzia kwenye muundo wa tume ya uchaguzi.

Alieleza mahakama jinsi alivyokamatwa akiwa Tarime na kufikishwa Dar es Salaam Novemba 4, 2025 ikiwa ni siku chache baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, baada ya kupitishwa Dodoma na kufikishwa Dar es Salaam, ambapo katika Kituo cha Polisi Oysterbay, aliwakuta mawakili wa serikali Nassoro Katuga, Job Mrema, Thawabu Issa na Cathbert Mbilinyi.

“Siku hiyo kulikuwa na watu wengi sana pale kituoni ambao walikuwa wamekamatwa, wengine wakiwa wamejeruhiwa...”

“Niliambiwa walikuwa wamekamatwa kwa saba bu ya vurugu za uchaguzi. Waliwekwa kwenye selo zao hadi kwenye korido. Hawa mawakili walikuwa pamoja na George Bagemu.

“Nilipeleka kwenye chumba ghorofa ya kwanza na kusomewa kwamba ninakabiliwa na kosa la ugaidi, nikidaiwa kuhusika na kuchoma vituo vya mwendokasi kuanzia Kimara hadi Ubungo...”

“Sikuwa tayari kuandika maelezo yangu. Wali-chukua tu majina yangu na mahali ninapoishi, kisha baada ya hapo wakanipeleka Kituo cha Polisi Mburahati ambapo niliwekwa humo kwa siku saba,” alisema.

Inaendelea Uk. 23

Kutoka Kesi ya Lissu ■

Ushahidi wa...

Inatoka Uk. 22

Alisema awali hakukamatwa kwa tuhuma ya ugaidi, bali kwa tuhuma ya kuvuka mpaka wakati akienda kuhudhuria mazishi ya Raila Odinga na alipewa tuhuma ya ugaidi baada ya kufikishwa Polisi Dodoma na ziliishia hewani.

Alisema kumekuwa na matukio ya kukamatwa kwa Lissu kwa kesi za uchochezi ambazo alizofunguliwa kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 ambazo ziliisha tu ambapo baadhi yake ilisemekana serikali haikuwa na nia ya kuziendeleza.

Alieleza kuwa mara kadhaa ratiba zao zimeingiliwa na polisi, watu kupigwa kwenye mikutano ya kampeni, wagombea kunyimwa fomu za matokeo, kura za uongo kuingizwa kwa maboksi na mabegi na askari polisi ambao walitakiwa kusimamia uchaguzi.

Heche ambaye wakati wote aliongozwa na Lissu, mtuhumiwa anyejitetea mwenyewe akisaidiwa kwa karibu na jopo la mawakili wake, alieleza kuwa katika uchaguzi wa Arumeru, aliyekuwa katibu wa USA River, Msafiri Bwambo, aliuawa kwa kuchinjwa kwa msumeno na watu waliosadikiwa kuwa wanachama wa CCM.

Alisema kwa Dar es Salaam, Kinondoni, Mwenyekiti wa Chadema Ananasi, Dani Yona aliu-



Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu, akiwa Mahakama Kuu - Masijala Ndogo ya Dar es Salaam baada ya kumaliza kumuongoza shahidi wake wa tano, makamu mwenyekiti wa chama hicho, John Heche, mwishoni mwa wiki. (Picha na Mpigapicha Wetu).

wa, pia mwanachama wao Akwilina Akwilini, ambaye Polisi ilikiri aliuawa kwa risasi na hakuna aliyekamatwa wala kushitakiwa.

Badala yake, alishitakiwa yeye na wajumbe wa kamati kuu ya chama chake, akiwemo John Mnyika, ambaye wakati huo alikuwa Katibu Mkuu; Freeman Mbowe ambaye alikuwa Mwenyekiti; Vincent Mashinji aliyekuwa Katibu Mkuu; Peter Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini na Ester Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini.

Wengine ni Halima Mdee, Mbunge wa Kawe; Ester Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini; na Salum Mwalimu, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar kwa makosa ya uchochezi na kushiriki kusanyiko lisilo na kibali.

Heche aliipitisha mahakama katika shambulio la risasi dhidi ya mwenyekiti ambaye kwa sasa anakabiliwa na shitaka la uhaini, Lissu ambaye wakati huo alikuwa makamu mwenyekiti na kulazimika kupatiwa matibabu nje ya nchi, kisha wao kuhukumiwa kifungo cha miezi sita au kulipa faini inayofikia shilingi milioni 300.

Alieleza kuhusu mauaji ya Alphonse Mawazo, ambaye alikuwa mgombea wa Jimbo la Busanda mwaka 2015 na mwenyekiti wa chama chake Mkoa wa Geita na kwamba wakati akifunga kampeni Nyamongo mwaka 2020, walivamiwa kwa risasi, ambapo watu wawili, Chacha Isangora na Chacha Gabir waliuawa na wengine kujeruhiwa.

Alisema akiwa katika shughuli za siasa, mdogo wake, Suguta Heche aliuawa ambapo awali alikamatwa Sirari mwaka 2018, akafungwa pingu mikono nyuma na kuchomwa sindano akiwa katika hali hiyo.

Heche alieleza baada ya tukio hilo, kulikuwa na madai ya jaribio la kumtupa ili ionekane amepata ajali au ameshambuliwa na watu wasiojulikana, lakini walinzi wa eneo waliona kilichokuwa kinaendelea, hivyo akarudishwa kituo cha polisi.

“RPC wa wakati huo alitoa taarifa kwa umma kwamba mdogo wangu ameuawa kikatili na kwamba hatua zingechukuliwa. Askari aliyekuwa anahusishwa na tukio hilo aliachiliwa na kuhamishwa kituo, na mpaka sasa ni mtumishi wa Jeshi la Polisi.

“Ninaamini mdogo wangu aliuawa kutokana na msimamo wangu wa kisiasa na kupinga maovu ya nchi hii, na kwamba tukio hilo lilikuwa ujumbe kwamba wanaweza kufanya lolote bila hatua za kisheria kuchukuliwa,” alieleza mahakama.

■ Kilinge cha Mawasiliano



Na Loth MAKUZA

Sifa ya wakili na mtaji wake usioonekana

FIKIRIA asubuhi moja umeamka na tatizo la kisheria linalohitaji wakili. Hutafungua tu orodha ya majina na kuchagua kibahati-bahati, bali utamuuliza rafiki, utatafuta jina fulani mtandaoni na utaangalia ni nani ambaye watu wanamwamini.

Kabla hata hujakutana na wakili uso kwa uso, tayari umekwishakutana na taswira yake ambayo ndiyo taswira ya kazi ya mawasiliano, yaani Public Relations.

Katika taaluma ya sheria, ambapo uaminifu, uadilifu na heshima ni kila kitu, taswira ya kampuni siyo jambo la kupuuzwa.


Wateja hawachagui wakili kwa bei pekee, bali wanachagua kwa imani, wanataka kujua kama huyu ni mtu wa kuaminika, mwenye ujuzi na mwenye rekodi njema.

Ndiyo maana mawasiliano mazuri siyo anasa kwa kampuni za sheria, ni uti wa mgongo wa biashara yenyewe.

Kampuni nyingi za sheria hazitumii vyema nguvu ya mawasiliano, zinafikiri kazi yao ni kushinda kesi tu na sifa itakuja yenyewe.

Lakini dunia ya leo siyo hivyo, kwani katika soko lililojaa mawakili wanaofanana, ni taswira ndiyo inayokutofautisha.

Kampuni inayoonekana mara kwa mara katika vyombo vya habari, inayotoa maoni ya kitaalamu, na inayoshiriki katika jamii, hujenga heshima inayowavuta wateja bila hata kuwaomba.



Wakili Peter Kibatala

Mawasiliano yanaisaidia kampuni kusimulia hadithi yake, thamani zake, mafanikio yake na namna inavyowajali wateja.

Hadithi hii, ikisimuliwa kwa uthabiti, hujenga daraja la imani kati ya kampuni na jamii.

Maoni mabaya mtandaoni, habari isiyo sahihi, au ujumbe uliopotoka unaweza kuharibu miaka ya kazi ngumu ndani ya siku moja.

Ndiyo maana kulinda sifa kunahitaji uangalifu wa kila siku. Ujumbe wa kampuni, kwenye tovuti, mitandao ya kijamii, na mawasiliano na wateja unapaswa kuwa mmoja na wenye mvuto.

Wataalamu wa mawasiliano husaidia kufuatilia kinachosemwa kuhusu kampuni, na kujibu kwa haraka na hekima pale panapotokea habari isiyo ya kweli. Ni bora kuzuia moto kabla haujawaka kuliko kuuzima baada ya kuteketeza nyumba.

Njia nzuri zaidi ya kampuni ya sheria kujijenga ni kuwafanya mawakili wake waonekane kama sauti za kuaminika katika fani zao.

Wakili anapoonekana akitoa uchambuzi kwenye vyombo vya habari vinavyoheshimika au akizungumza kwenye jukwaa la kitaifa, jina lake hubadilika.

Hakuonekani tena kama mtoa huduma wa kawaida, bali kama mtaalamu anayeongoza.

Mawakili hushughulikia mambo nyeti, kesi tata, tuhuma na mabishano ambayo yakiingia hadharani yanaweza kutikisa kampuni nzima. Wakati kama huu, mawasiliano ndiyo ngao.

Mkakati mzuri wa mawasiliano ya dharura huhakikisha kampuni inajibu kwa utulivu, kwa ujumbe mmoja, na kwa wakati muafaka, bila kukurupuka wala kunyamaza kimya kupita kiasi.

Zama zimebadilika, kuwa na mkakati wa mawasiliano siyo tena hiari kwa kampuni za sheria, ni hitaji la lazima.

Wateja wa leo wanachunguza kabla ya kuchagua, na taswira yako ndiyo inayozungumza kabla wewe hujazungumza.

Kampuni inayowekeza katika mawasiliano hujenga imani, huonekana na hulinda sifa yake katika kila hatua. Mwishoni, swali siyo kama kampuni yako inahitaji mawasiliano, ni kama uko tayari kuiacha taswira yako ijipange yenyewe, au utaamua kuiongoza.

Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz

Na Emmanuel JACOB



Afya ya Kimwili ■

Usimfanyie masaji ya nguvu mgonjwa wa kiharusi

KIHARUSI ni dharura kubwa ya kitiba inayotokea pale mzunguko wa damu kwenda kwenye ubongo unapokatika au pale mshipa wa damu unapopasuka.

Katika jamii zetu, mara nyingi mgonjwa anapopooza kutokana na kiharusi, ndugu hukimbilia kumfanyia ukandaji (masaji) wakati mwingine kwa nguvu sehemu mbalimbali za mwili huku wakiamini itarudisha utendaji kazi wa misuli na mwili.

Hata hivyo, jambo hili linaweza kuleta madhara kwa mgonjwa badala ya kumsaidia.

Mara mtu anapopata kiharusi, mabadiliko hutokea kwenye mishipa ya damu inayopeleka damu kwenye ubongo ambayo inakuwa imepasuka au kuvimba.

Katika hali hii tunahitaji muda wa kupona na kurejea kwenye hali yake. Na taarifa zinazotoka maeneo mbalimbali kwa mfano sauti, miguso, au mitetemo ni muhimu ikawa kwenye hali ambayo inachochea uponyaji.

Kukanda kwa nguvu au kwa kina (deep, vigorous massage) kunaweza kusababisha kuvimba kutokana na damu kuvilia (blood clots) na maumivu makali kwenye viungo mbalimbali.

Usilazimishe, badala ya kutumia nguvu nyingi, wataalamu hushauri kutumia mbinyo kidogo na wa upole sana (light pressure) ili kuepuka kuongeza msongo kwenye mishipa ya damu.

Kwa safu yetu wiki hii, tutaangalia kuhusu dhana potofu zilizosambaa kwenye jamii kuhusu massage hasa kwa wagonjwa waliopatwa na kiharusi:

Dhana potofu ya kwanza; Masaji peke yake inaweza “kutibu” au kurejesha utendaji kazi wa kimwili baada ya kiharusi. Ukweli ni kwamba; Masaji ni tiba ya ziada tu (complementary therapy).

Hainusuru wala kurejesha mfumo wa neva ulioharibika, na haiwezi kuchukua nafasi ya mbinu kama tiba ya mazoezi (physical therapy), tiba kwa vitendo (occupational therapy), au tiba inayomwezesha mgonjwa kuzungumza tena (speech therapy).

Dhana potofu ya pili; Masaji ya nguvu na ya kina “inaondosha” kukaza na kukakamaa kwa misuli. Ukweli ni kwamba; Kukakamaa au kukaza kwa misuli (spasticity), kulazimisha massage ya nguvu au kuvuta misuli kwa nguvu kunaweza kusababisha majeraha makubwa kwenye tishu.

Kukabiliana na hali hii ya kukakamaa au kukaza inahitaji mbinu za taratibu, pamoja na matibabu ya dawa, na mazoezi maalum kutoka kwa mfiziotherapia.

Dhana potofu ya tatu; Lazima usubiri muda unaofaa na kushauriwa kitaalamu (kama wiki sita) kabla ya kuanza masaji. Ukweli ni kwamba; hakuna kanuni moja ya muda kwa kila mtu. Ili kuanza inategemea sana na utulivu wa afya ya mgonjwa, aina ya kiharusi, na idhini ya daktari.

Hata hivyo, masaji haipaswi kufanyika kabisa wakati bado mgonjwa akiwa katika hali mbaya na isi-yostahimilika (acute stroke).

Dhana potofu ya nne; Masaji inatoa “sumu” mwilini. Ukweli ni kwamba; kulingana na Chama cha Tiba ya Massage cha Marekani (American Massage Therapy Association), hakuna ushahidi wa kisayansi unaothibitisha kuwa masaji inatoa sumu kutoka kwenye misuli kwenda kwenye mzunguko wa damu.

Masaji hapaswi kutazamwa kama muujiza wa kurejesha viungo vilivyopooza. Njia salama zaidi ya kumsaidia mgonjwa wa kiharusi ni kufuata mpango wa matibabu uliowekwa na madaktari na kufanya mazoezi ya tiba viungo na mazoezi (physiotherapy) chini ya usimamizi wa wataalamu waliosomea kazi hiyo.

Masaji hapaswi kutazamwa kama muujiza wa kurejesha viungo vilivyopooza. Njia salama zaidi ya kumsaidia mgonjwa wa kiharusi ni kufuata mpango wa matibabu uliowekwa na madaktari na kufanya mazoezi ya tiba viungo na mazoezi (physiotherapy) chini ya usimamizi wa wataalamu waliosomea kazi hiyo.

Mwandishi: Emmanuel Jacob, Afisa Mfiziotherapia (Mwenyekiti wa Tanzania Physiotherapy Initiative). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob



Bustani ya Sheria**Na Wakili Karim Gabriel Mussa**

Ardhi yako imevamiwa?

Usifanye kosa hili la kusubiri

IKIWA una mgogoro wa ardhi na ukaendelea kulalamika kwa viongozi wa kijiji kwa miaka mingi, hatua hiyo pekee haisimamishi ukomo wa muda wa kisheria (limitation period).

Katika hukumu hii, mrufani (appellant) alieleza kuwa aligundua madai ya mjibu rufaa (respondent) dhidi ya ardhi yake mwaka 2011.

Baada ya hapo, aliwasilisha malalamiko kadhaa kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Mang'onyi, lakini mashauri rasmi ya kisheria yalianza mwaka 2025.

Mahakama Kuu ilibaini kuwa kipindi hicho kili kuwa takriban miaka 14, wakati sheria ya kudai au kurejesha ardhi (recovery of land) ikiekeza ukomo wa muda wa miaka 12.

Katika kesi ya Elisha Kyang'u Sungi v. Israel Joseph (Land Appeal No. 7723/2026, High Court Dodoma), Jaji: Mheshimiwa Hassan, J.

Elisha Kyang'u Sungi alidai kuwa alipata eneo la ardhi lenye ukubwa wa ekari 25 mwaka 1982 baada ya kulifyeka na kuanza kulitumia. Mwaka 1990, aliondoka eneo hilo na kumuachia baba yake, Kyangu Khome, aliyefanya shughuli za kilimo na ufugaji hadi alipofariki dunia mwaka 2008.

Hata hivyo, mnamo mwaka 2011, Elisha alitarifiwa na mtu aitwaye Apolinary kuwa kuna mtu mwingine aliyekuwa anadai umiliki wa ardhi hiyo. Hapo ndipo msingi wa mgogoro ulipoanzia.

Sasa badala ya kufungua mashauri rasmi ya kisheria au ya kimahakama mara moja, aliendelea kuripoti mgogoro huo kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Mang'onyi kwa nyakati tofauti. Pamoja na malalamiko hayo, mgogoro haukupata usuluhishi.

Hatimaye, mnamo mwaka 2025, ndipo alipoanzia mashauri rasmi kwanza katika Baraza la Ardhi la Kata (Ward Tribunal) na baadaye katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya (District Land and Housing Tribunal).

Hapa ndipo suala kuu la kisheria lilipoibuka, je, muda wa kufungua kesi ulikuwa umekwisha kisheria?

Mahakama ilirejelea Sheria ya Ukomo wa Muda, Sura ya 89 (R.E. 2023) (Law of Limitation Act, Cap. 89 R.E. 2023) Kifungu cha 4 kinaeleza kuwa hesabu za muda wa ukomo huanza pale tu haki ya kuchukua

hatua za kisheria inapojitokeza (right of action accrues).

Kipengele cha 22, Sehemu ya I ya Jedwali kinaweka ukomo wa miaka 12 kwa mashauri ya kurejesha au kudai ardhi (suit for recovery of land).

Kutokana na msingi huo, suala kuu halikuwa tu kujua kama Elisha alikuwa mmiliki halali, bali alijua lini kwa mara ya kwanza kuwa kuna mtu mwingine anayedai haki juu ya ardhi yake?

Majibu yalipatikana kutoka kwenye ushahidi wa mrufani mwenyewe. Alikiri kuwa alifahamu uwepo wa madai hayo yanayokinzana na umiliki wake (adverse claim) mwaka 2011, na ndipo alipoanza kuwasilisha malalamiko kwa serikali ya kijiji.

Mahakama ilifafanua kuwa, mara tu alipogundua kuwa kuna mtu anayepinga umiliki wake, mazingira yaliyotoa haki ya kufungua shauri (cause of action) yalikuwa yameshajitokeza tayari.

Kwa hiyo, saa ya ukomo wa muda (limitation clock) ilianza kuhesabu kuanzia mwaka 2011.

Wakati sheria inataka shauri lifunguliwe ndani ya miaka 12, mrufani alifungua shauri lake baada ya miaka 14 kupita. Kwa hiyo, hata kwa kuzingatia maelezo yake mwenyewe, alikuwa ameshapitiliza muda uliolekwa na sheria.

Je, malalamiko katika serikali ya kijiji yalisimamiwa saa ya sheria?

Jibu ni Hapana na hili ndilo somo kuu la kisheria katika kesi hii.

Mahakama ilibaini kuwa kufanya jitihada za kiseri au kiutawala (administrative settlement) kupitia viongozi wa kijiji hakuondoi wala kuzuia haki ya msingi ya kufungua shauri iliyokwisha kujitokeza (cause of action), na wala haisimamishi saa ya kisheria (statutory clock).

Kwa maneno mengine, kutoa taarifa au kulalamika kwa viongozi wa kijiji hakumaanishi kuwa muda wa ukomo wa kisheria unaanza upya kila unapolalamika.

Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karimbinmussa@gmail.com

Na Rashid MTAGALUKA



Hoja Yangu ■

Kwa nini tunapenda uzinduzi kuliko matokeo?



CAG,
Dkt. Charles
Kichere

KUNA jambo moja ambalo Tanzania tunapaswa kuanza kulitafakari upya. Kwa nini tunafurahia sana kuzindua miradi, lakini wakati mwingine tunasahau kuuliza matokeo yake?

Kuweka jiwe la msingi, kukata utepe, kupiga picha na kutoa hotuba ni sehemu ya kawaida ya utekelezaji wa miradi, lakini maendeleo ya kweli hayapimwi kwa ukubwa wa sherehe ya uzinduzi. Yanapimwa kwa namna mradi unavyobadili maisha ya wananchi.

Hili siyo suala la hisia. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka wa fedha 2024/25 imeonyesha changamoto kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Kwa mfano, miradi 47 yenye thamani ya Shilingi bilioni 105.56 katika mamlaka za serikali za mitaa ilichelewa zaidi ya muda wa mikataba au ilisimama kwa zaidi ya siku 90. Huku miradi 671 yenye thamani ya Shilingi bilioni 79.17 katika halmashauri 47 ilikuwa haijakamilika.

Hii ndiyo sehemu ambayo mjadala wetu unapaswa kuanzia. Mradi wa shule unaweza kuzinduliwa kwa mbwembwe, lakini kama madarasa hayatoshi, maabara haifanyi kazi au wanafunzi hawapati mazingira bora ya kujifunzia, tunapaswa kujiuliza kama tumefikia lengo.

Au hospitali inaweza kuzinduliwa, lakini kama haina vifaa, haina watumishi au haina dawa za kutosha, jengo pekee haliwezi kuitwa mafanikio kamili. Hii ndiyo Hoja Yangu.

Vivyo hivyo, barabara inaweza kukamilish-

wa na kuzinduliwa, lakini kama baada ya muda mfupi inanza kuharibika kwa sababu ya ubora duni wa ujenzi, swali halipaswi kuwa nani alizindua, bali kwa nini fedha za wananchi hazijaleta thamani iliyokusudiwa? Hii ndiyo Hoja Yangu.

Hata katika miradi mikubwa, changamoto hii ipo. CAG alibaini, kwa mfano, madai ya wakandarasi yaliyocheleweshwa kulipwa katika miradi mbalimbali, yakiwamo Sh14.05 bilioni katika Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road na Shilingi bilioni 11.75 katika mra-di wa maji.

Tatizo si kuwa na miradi mingi. Tatizo ni kuhakikisha kila shilingi iliyowekezwa inazalisha thamani inayokusudiwa. Hii ndiyo Hoja Yangu.

Hapa ndipo tunapohitaji kubadili pia utamaduni wetu wa kushangilia mafanikio. Wananchi wanapaswa kupewa taarifa si tu wakati mradi unapozinduliwa, bali pia kuhusu gharama yake, muda uliopangwa kukamilika, changamoto zilizojitokeza na faida ambayo wananchi wanatarajiwa kupata. Hii ndiyo Hoja Yangu.

Tunapaswa kubadilisha namna tunavyopima mafanikio. Badala ya kuuliza, “Umezindua miradi mingapi?”, tuulize, “Miradi hiyo imekamilika mingapi? Inafanya kazi? Wananchi wanaufaika kwa kiasi gani?” Hii ndiyo Hoja Yangu.

Hapo ndipo uwajibikaji unapokuwa na maa-na. Serikali, viongozi na taasisi zetu wanastahili pongezi kwa miradi inayotekelezwa, lakini pongezi hizo hazipaswi kuwa mwisho wa safari. Uzinduzi ni mwanzo; matokeo ndiyo ushindi.

Tanzania inahitaji utamaduni mpya wa maendeleo, utamaduni unaopima si ukubwa wa jukwaa la uzinduzi, bali ukubwa wa mabadiliko yanayobaki baada ya wageni kuondoka.

Kwa sababu hatimaye, mwananchi hahitaji picha ya kiongozi akikata utepe. Anahitaji kuona maisha yake yamebadilika. Hii ndiyo Hoja Yangu.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com

■ Habari

ACT, CCM ‘mwendomdundo’ maridhiano



Rais Mwinyi

Na Jabir IDRISSE, Zanzibar

RAIS wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi ameitangaza Kamati ya Pamoja ya Majadiliano itakayofuatilia na kuchambua mambo yaliyokubaliwa na vyama viwili vya siasa vilivyokamilisha mazungumzo ya kuondoa mvutano wa kisiasa uliobuka tena baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka jana.

Kamati hiyo itaongozwa na wenyevit wawili, mmoja kila upande kati ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha ACT Wazalendo.

Taarifa ya Ikulu ya Zanzibar, iliyotolewa jana na Katibu wa Baraza la Mapinduzi (BLM) na Katibu Mkuu Kiongozi, Mansura Mossi Kassim, Rais amemteua Abdi Mahmoud Abdi kutoka CCM na Omar Ali Shehe kutoka ACT Wazalendo kuiongoza kamati itakayokuwa na wajumbe kumi.

Wateuliwa hao wawili ambao wote kwa sasa ni manaibu katibu wakuu wa vyama vyao upande wa Zanzibar, wanakuwa wajumbe na wakati huohuo wenyevit wenza wa kamati hiyo inayotarajiwa kuzinduliwa rasmi leo katika hafla itakayofanyika

Othman
Masoud
Othman

Ikulu mjini hapa majira ya Saa 5 asubuhi.

Wajumbe wengine wanaounda kamati hiyo ni Dkt. Khalid Salum Mohamed, Najma Murtaza Giga, Masoud Ali Mohamed na Mgeni Hassan Juma wanaotoka CCM.

Dkt. Khalid ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi anayewakilisha jimbo la uchaguzi la Donge, Wilaya ya Kaskazini A, Mkoa wa Kaskazini Unguja, na pia Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwenye serikali iliopo ambayo Dkt. Mwinyi aliiunda baada ya uchaguzi huo wa Oktoba 2025.

Masoud naye ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuteuliwa na rais. Mgeni ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia Viti Maalum wanawake, na ameendelea kuwa Naibu Spika katika Baraza la Wawakilishi kwa kipindi cha tatu mfululizo sasa.

Giga naye ni Mbunge wa Viti Maalum akiwa pia mmoja wa wenyevit wanaomsaidia Spika na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongoza vikao.

Wajumbe wanne wengine kutoka ACT Wazalendo ni Omar Said Shaaban, Fatma Abdulhabib Fereji, Said Ali Mbarouk na Mohamed Nur Mohamed. Omar ambaye kitaaluma ni mwanasheria na wakili nchini, ndiye Mwanasheria Mkuu wa ACT wakati Fereji, mwalimu kitaaluma, kwenye chama ni Katibu wa Ngome ya Wanawake.

Aidha, wote Omar na Fereji, pamoja na Mbarouk, waliwahi kuwa mawaziri katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Taarifa ya Ikulu pia imetaja kuwepo kwa makatibu wa kamati ambako walioteuliwa ni Mwalim Ali Mwalimu Seif Khamis Mohamed. Na imeundwa sekretatieti ya kamati ambayo taarifa inawataja wajumbe wake kuwa ni Hamid Saleh Mhina, Mohamed Yussuf Nuh, Ali Salim Khamis na Abdalla Mussa Hija.

Kutangazwa kwa kamati hiyo ya pamoja ni hatua muhimu ya kuendeleza ufuatiliaji wa makubaliano yaliyofikiwa na CCM na ACT Wazalendo baada ya mazungumzo yaliyochukua miezi minane kuanzia Novemba mwaka jana - 2026, yaliyofikia tamati kwa kutolewa tamko la pamoja Julai 9 Julai, mwaka huu.

Makala ya Afya ■

Kudamka kunavyokatiza umakini wa watoto



Na Dickson KAPUNGU, Songwe

KUWAHI shule alfajiri ni sehemu ya maisha ya kila siku kwa wanafunzi wengi. Baadhi yao huamka mapema kujiandaa, kutembea umbali mrefu au kutumia usafiri wa umma.

Ingawa wazazi na walimu huona utaratibu huo kuwa njia ya kujenga nidhamu, uwajibikaji na kuheshimu muda, unaibua swali muhimu; Je, ratiba za shule zinazingatia afya na mahitaji ya usingizi ya mtoto?

Baadhi ya wanafunzi wa Mkoa wa Songwe wanasema hushindwa kuzingatia masomo kutokana na uchovu. Huamka saa 11 alfajiri baada ya kuchelewa kulala kwa sababu ya muda mrefu wanaotumia shuleni na majukumu ya nyumbani.

Marry Ayubu Kinyamagoha, mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Tunduma, anasema hutoka shuleni saa 12 jioni. Akifika nyumbani huwasaidia wazazi kuandaa chakula hadi saa nne usiku, kisha huamka saa 11 alfajiri. Ratiba hiyo humpa takribani saa saba tu za usingizi.

Laban Zakaria, mwanafunzi wa shule hiyo, anasema kuamka mapema baada ya kulala usiku humfanya asinzie darasani na kushindwa kufuatilia mafundisho vizuri.

Pia anakabiliwa na hatari ya kukimbizwa na mbwa ambao hawajafungiwa wakati anapoelekea shuleni alfajiri.

Kwa mujibu wa takwimu za Vituo vya Marekani vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, CDC, watoto wenye miaka sita hadi 12 wanahitaji saa tisa hadi 12 za usingizi kila baada ya saa 24, huku vijana wa miaka 13 hadi 18 wakihitaji saa nane hadi 10.

Kukosa usingizi wa kutosha huhusishwa na matatizo ya umakini, tabia, afya ya akili na ufaulu.

Mapitio ya utafiti yaliyochapishwa mwaka 2016 katika jarida la Sleep Medicine Reviews yalibaini kuwa kuchelewesha muda wa kuanza shule kwa dakika 25 hadi 60 kuliongeza usingizi wa vijana kwa dakika 25 hadi 77 kwa usiku wa siku za masomo.

Akizungumza kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Dkt. Abdulazack Haji anasema usingizi wa muda mfupi huathiri uwezo wa kufikiri, umakini, kumbukumbu na utatuzi wa matatizo.

Kwamba unaweza pia kusababisha mabadiliko ya hisia, ikiwamo mtoto kukasirika bila sababu.

“Usingizi wa kutosha ni muhimu kwa ukuaji, afya ya akili, kumbukumbu na uwezo wa kuzingatia. Mtoto anayeamka mapema lazima apate muda wa kutosha wa kulala,” anasema.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Tunduma, Tutindaga Mwakibete, anasema uchovu huonekana darasani kupitia kusinzia, kupungua kwa umakini na uwezo mdogo wa kukumbuka.

Shuleni kwake hali hiyo hujitokeza zaidi katika masomo ya mchana kutokana na njaa, lakini pia na usingizi kwa kuwa watoto wanachelewa kulala wanapofika nyumbani. Anawashauri wazazi kuacha watoto walale mapema na pia kuchangia chakula shuleni ili kupunguza uchovu.

Wazazi wanashauriwa kupanga muda wa kazi za shule na majukumu ya nyumbani, kupunguza matumizi ya simu, televisheni na michezo ya video kabla ya kulala, na kuweka muda maalumu wa mtoto kupanda kitandani kulala.

Shule nazo zinapaswa kuangalia zaidi ya mahudhurio na kuchelewa. Ushirikiano wa wazazi, walimu, wataalamu wa afya na watunga sera unahitajika kusawazisha nidhamu, safari, chakula na usingizi.

Sasa swali kubwa si kama mtoto amewahi shule pekee, bali kama amelala vya kutosha kujifunza vizuri na kulinda afya yake.

■ Barua za Wasomaji



Tunakaribisha barua. Tuma kupitia

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba;
+255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

Wahudumu wa afya Momba hatujalipwa stahiki

Mhariri,

SISI ni wahudumu wa afya ngazi ya jamii wilayani Momba, hatujalipwa posho zetu kwa miezi nane sasa.

Mara ya mwisho tulilipwa posho kiasi baada ya kufikisha suala letu kwa Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa, ambapo walitoa maelekezo tulipwe na tunadai kuanzia Januari mwaka huu hadi sasa mwezi huu wa Septemba.

Kiukweli tunateseka kwa sababu tunatembea umbali mrefu lakini wahusika hawajali kuhusu stahiki zetu, tukiuliza wanadai kuna changamoto ya mfumo. Inawezekanaje kwa miezi yote hiyo minane mfumo uwe na changamoto? Sisi hatuamini hivyo lakini tunachooona ni kwamba hawatujali.

Tunaomba kupitia gazeti lako la Pambazuko utupazie sauti maana tunateseka na ugumu wa maisha huku familia zinatutegemea.

Ni sisi,

**Wahudumu wa afya ngazi ya jamii,
Wilaya ya Momba-Tunduma**

Tamisemi ifanyie kazi kero ya watumishi wanaohama

Mhariri,

NALETA kero yangu kwa niaba ya watumishi wengine kwamba mtumishi anapohama asilimia za utendaji katika mfumo wa Pepmis zinarudi zero.

Hiyo inatokea mtumishi anapotoka halmashauri moja kwenda nyingine hata kama alikuwa amefikisha asilimia 60 alipotoka, anapohama anaanza upya.

Utaratibu huo unafanya mtumishi kuwa na muda mfupi wa kufikisha asilimia zinazotakiwa, kwani muda anapohama tathmini inakuwa inaendelea, matokeo yake, baadhi yao hukwama kupanda daraja na kupata stahiki zao.

Tunaomba Tamisemi ilifanyie kazi suala hili, kwamba anayehama aende na alama zake kwa kuwa muajiri ni mmoja.

**Evarist Jacob,
Mtumishi wa umma.
Songwe**

Serikali ituambie alipo Dkt. Nchimbi

Mhariri,

NIKIWA raia wa Tanzania nina haki ya kufahamu alipo aliyekuwa makamu wetu wa rais, Dkt. Emmanuel Nchimbi, kwa sababu tangu alipojiuzulu nafasi hiyo na baadaye akavuliwa uanachama na chama chake, hajaonekana hadharani.

Kwa kuwa minongoŋo imekuwa ni mingi kuhusu usalama wa kiongozi huyo, ni vyema sasa serikali ikasaidia kutoa taarifa alipo ili kuvunja sintofahamu hii.

Tunasikia na kuona taarifa nyingi zikisambaa kuhusu Dkt. Nchimbi huku wengine wakisema eti hajulikani alipo.

Tunajiuliza pamoja na uvumi huo, kwanini familia yake na serikali wako kimya? Watanzania wana haki ya kufahamu alipo kiongozi huyo ambaye amekuwa akipinga matukio mabaya yaliyopata kutokea katika nchi yetu na mara nyingi ameonekana akiwa upande wa wananchi.


Kwa kuwa amekuwa upande wetu wananchi, hivyo ni haki yetu kufahamu alipo.

Nawaomba Watanzania na vyombo vya habari, kwa umoja wetu tupaze sauti kwa kuishinikiza serikali iseme alipo kiongozi huyo.

**Augusta Herman,
Unga Limited, Arusha.**

Harambee... ■

Bati/ Mtu, Mtu Bati HATUCHOKI!



Changia kupitia

NMB A/C NO 31910046325

ELCT KARAGWE IRON SHEET PROJECT

CRDB A/C NO 0150764151900

UWAKILI PROJECT ELCT KAD

Mawasiliano:

0754 742 423

Askofu Benson K Bagonza

■ Vituko vya Wakubwa

‘Maajabu’ ya Rais Mobutu akiwa Ikulu - III



Na Mwandishi WETU

TUNAENDELEA simulizi na visa, vituko na mikasa vilivyofanywa na Rais wa Zaire (sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo), Mobutu Sese Seko Kuku wa Zabanga.

Kiongozi aliyechukua madaraka baada ya mapinduzi, miaka michache baada ya kifo cha rais wa kwanza baada ya wakoloni, Patrice Lumumba.

Mobutu, kwa lugha ya vijana, alikuwa ‘chuma’ kweli. Nani angethubutu kumnyoshea kidole katika zama zake?

Hata hivyo, hakuna marefu yasiyokuwa na ncha, hatimaye Mobutu aliyekuwa mtu wa ‘kula bata’ na mvinyo kutoka Paris Ufaransa, Monaco na Rabat alifika mwisho.

Siku chache kabla ya kuondolewa madarakani kupitia mapinduzi yaliyoongozwa na Laurent-Désiré Kabila, waliomshuhudia Mobutu -

siku chache kabla ya kupinduliwa kwake mwaka 1997, walisema alikumbwa na wasiwasi mkubwa, kiasi cha kushindwa kula kwa siku kadhaa.

Ikumbukwe kuwa kabla ya kupinduliwa alianza kukumbwa na majaribio kadhaa ya mapinduzi na baadaye akapata dhoruba ya ugonjwa wa kansa ya korodani.

Kipindi ambacho urais wake uliingia kwenye majaribio ya kupinduliwa na uasi kuongezeka ni miaka ya 1992 hadi 1997, katika kipindi hicho urais wake haukuwa wa kula bata tena, kwani hata yeye mwenyewe aliona wazi kuwa “Zaire siyo mali yake tena.”

Ni kipindi ambacho hata askari ambao walikuwa watiifu kwake, walianza kumsaliti.

Mwaka 1986, Mobutu alianza kutetea ufalme wake, aliunda kikosi maalumu cha ulinzi wake binafsi kilichojulikana kwa jina la DSP, ambacho kilikuwa katili kwa kila aliyeshukiwa kuwa “mpinzani.”

DSP kilikuwa na wanajeshi wanaokadiriwa kufikia 10,000, huku wengi wao wakitoka kabila la Mobutu la Ngbandi. Wanajeshi hao walikuwa wanapewa mafunzo nchini Israel, pamoja na kuwa na vifaa vya kisasa kabisa.

Ikumbukwe kuwa kabla ya Mobutu, Zaire iliongozwa na rais wake wa kwanza aliyeitwa Joseph Kasavubu, huyu alilindwa na mwanajeshi mmoja au wawili.

Mara nyingi alipokuwa akitembea hakuwa na msafara wowote.

Wanajeshi wa DSP walilipwa vizuri zaidi na Mobutu, na aliwaamini sana. Kila alipokwenda kuishi kijijini kwake ambako baadaye uligeuka kuwa mji, huko Gbadolite alisindikizwa na wanajeshi 300 ikiwa ni kwa ajili ya ulinzi tu.

Ijumaa ya Mei 16, 1997, Mobutu alinusurika kufa, wakati akiwa Uwanja wa Ndege wa Ndiji karibu na Kinshasa. Akiwa ndani ya ndege, dakika za mwisho ndege ianze kuruka, mkuu wa usalama wa Mobutu, Kanali Motoko alipokea taarifa ya kiintelijensia kuwa kwenye shamba kubwa lililokuwa karibu na uwanja huo kuna gari la jeshi aina ya jeep likiwa na vifaa vyote vya kudungulia ndege ya Mobutu.

Inaendelea Uk. 33

Vituko vya Wakubwa ■

‘Maajabu’ ya Rais...

Inatoka Uk. 32

Kanali Motoko alimwambia rubani wa ndege hiyo ya rais abadili uelekeo wa kurusha ndege hiyo, lakini rubani alikataa akidai upepo hauruhusu kufanya hivyo.

Kanali Motoko anamwambia Mobutu jambo hilo, Mobutu akamwamuru rubani afuate uamuzi wa mkuu wa usalama.

Ndege ilibadili uelekeo, na wale wanajeshi waliokuwa wakisubiri waitungue walihaha na kuanza kukimbia karibu na ndege inakorukia ili waitungue, lakini walipata ajali na wote walikufa papo hapo. Mobutu akaenda zake salama Gbadolite ‘kula bata’.

Jaribio la pili kubwa

Baada ya kufika huko kijijini kwake, mwanajeshi mmoja kutoka kikosi cha DSP, aliomba wasaa wa kumnong’oneza Mobutu na alipaswa kuanzia kwa mkuu wa kikosi hicho ili kupata ruhusa.

Alipofika kwa mkuu huyo, Kanali Motoko alikataa, kumruhusu na baadaye aliamuru askari huyo akaguliwe mwili mzima. Baada ya ukaguzi alikutwa kajifunga mabomu.

Alipoulizwa ya nini anapanga kumuua Rais Mobutu na ametumwa na nani kufanya hivyo? Alijibu kwa kifupi tu kwamba alichoshwa na tabia za Mobutu hivyo alitaka ajitoe muhanga ili wafe wote.

Siku moja msaidizi wa mlinzi mkuu wa Mobutu, Meja Ngani Yanda Mokomba, wakati anafanya ukaguzi wa njia, akiwa huko alikutana na kikosi cha DSP kikirudi kutoka Gbadolite huku wakiimba “Mobutu msaliti, ndugu yake Nzimbi amekimbilia Brazaville katuacha sisi tufe, twendeni tukamkamate Mobutu.”

Meja Ngani alikwenda chumbani kwa Mobutu, alimkuta kiongozi huyo kavaa shati lake bila fulana, na viatu bila soksi, akamwambia watoroke. Mobutu akakataa, akidai anataka kufia nyumbani kwake. Mobutu anawaambia mlinzi huyo awamchukue mkewe na pacha wa mkewe, yeye wamuache afie hapo.

Meja Ngani alikataa kumwacha bosi wake.


Alimbeba Mobutu mgongoni baada ya kumuomba samahani kwa sababu kulikuwa na sheria kali kwamba hairuhusiwi mlinzi wa rais kumshika rais.

Mobutu alibebwa mgongoni huku pia akiwa dhaifu kutokana na maradhi ya kansa ya kibofu yaliyoanza kumtafuna.

Meja Ngani ambaye pia alikuwa rubani, alipofika uwanja wa ndege ambao haukuwa mbali na kwenye hekalu lake, hakukuta ndege ya Rais Mobutu, aliamua kuiteka ndege ya Urusi iliyokuwa imeleta vifaa vya kijeshi kwa Jonas Savimbi (Savimbi alikuwa rafiki mkubwa wa Mobutu), wakati huo alikuwa amempa hifadhi ya ardhi ya Congo kutumika kuihujumu serikali ya Angola.

Makala haya yaliyoandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali ikiwamo mitandao, yataendelea wiki ijayo.





Ujasiri humjenga mtoto



BILA shaka u mzima msomaji wangu wa safu ya uhusiano. Wiki hii nitazungumza umuhimu wa mtoto kufundishwa ujasiri.

Ujasiri ni jambo muhimu ambalo mzazi au mlezi anapaswa kulipanda kwa mtoto tangu wakati wa utoto wake.

Mtoto jasiri anakuwa mtu anayeweza kukabiliana na changamoto za maisha bila kukata tamaa.

Ujasiri unampa mtoto uwezo wa kutatua matatizo yake mwenyewe badala ya kulia au kukimbia, lakini pia unampa uthubutu wa kujaribu tena hadi kufaulu.

Unamjengea pia tabia ya kutokata tamaa shuleni au mahali popote atakapokuwa, pia humpunguzia hofu na wasiwasi.

Watoto wengi huogopa kuuliza maswali, kuzungumza mbele ya watu, au kukataa mambo mabaya waliyofanyiwa au kufanya.

Mzazi anapomfundisha mtoto kuzungumza ukweli na kusema 'hapana' anampa ngao dhidi ya udanganyifu na vitisho.

Humjenga kuwa kiongozi bora wa kesho. Mtoto jasiri akiwa mahali popote hutetea

mwenzie kwa mambo watakayokabiliwa nayo na katika jamii anakuwa mtu wa kutoa suluhu, siyo kulalamika.

Hata viongozi wengi wakubwa tulionao sasa historia ya utoto wao huonyesha kwamba walianza kuwa na ujasiri.

Pamoja na mambo mengine hali hiyo humlinda mtoto. Watoto waoga ni rahisi kudanganywa au kuteswa kimya, lakini mtoto aliyefundishwa kufanya maamuzi pale anapofanyiwa jambo mfano kupiga kelele anapoteswa au kupatwa na kitu kisicho cha kawaida ili kujinusu hawezi kutetereka.

Jamii inapaswa kuelewa kwamba kumfundisha mtoto ujasiri si kumfanya awe mkorofi bali kunamfanya awe na moyo wa uthubutu!

Mzazi au mlezi anayepanda mbegu ya ujasiri leo kwa mtoto wake anavuna mtu mzima asiyeogopa maisha kesho. Ujasiri ni kuchagua kufanya lililo sahihi hata moyo ukitetemeka.

Tukutane wiki ijayo, penye majaaliwa.

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.

Mitindo & Urembo ■

Fascinator: Pambo la kichwani linalobamba

FASCINATOR ni miongoni mwa vifaa vya urembo vinavyoweza kuongeza mvuto wa pekee katika muonekano wa mwanamke.

Tofauti na kofia za kawaida, kazi ya kuu fascinator ni kurembesha na kuongeza nakshi kwenye vazi lako.

Ili uonekane wa kisasa ni muhimu uzingatie mpangilio wake kulingana na aina ya vazi, rangi na mtindo wa nywele.

Fascinator inaweza kuwekwa upande mmoja wa kichwa, mbele kidogo au juu kulingana na umbo la uso na muundo wake.

Kwa mavazi yenye rangi tulivu, fascinator yenye rangi au mapambo yanayovutia inaweza kuongeza mvuto.

Pia fascinator yenye mapambo mengi inapaswa kuvaliwa na mavazi yasiyo na mapambo mengi ili kuepuka mwonekano uliozidi.

Kwa hafla kama harusi au sherehe yoyote, fascinator inaweza kuambatana na gauni, suti au vazi la 'two-piece'.



Faida za manjano kwenye ngozi

MANJANO (turmeric) ina faida kubwa kwenye ngozi ikiwemo kung'arisha, kutibu chunusi na kupunguza mafuta usoni.

Namna ya kutumia;

* Unaweza kuchanganya unga wa manjano kwenye asali au maziwa ili kutengeneza mchanganyiko wa kupaka

usoni.

* Changanya kijiko kimoja cha manjano na asali au maziwa kwenye chombo, koroga vizuri hadi uwe uji mzito

* Hatua inayofuata paka usoni, acha mnyanganyiko huo ukae usoni kwa dakika 15 hadi 20. Fanya hivyo mara mbili kwa wiki kwa matokeo mazuri zaidi.



■ **Burudani**

Kajala kumshtaki Mwijaku, adai fidia ya mil 200/-

Na Mwandishi WETU

MWIGIZAJI wa filamu, Kajala Frida Masanja kupitia mawakili wake, amemtaka Burton Mwemba maarufu Mwijaku kuacha mara moja kutoa, kuchapisha au kusambaza kauli anazodai zinamdhalilisha na kumchafulia jina.

Katika barua ya kisheria iliyotumwa kwa Mwijaku, mawakili hao wamedai kuwa video na kauli zake zinazomhusu Kajala zimekuwa zikisambaa kwenye mitandao ya kijamii na zinaweza kuharibu heshima, sifa na

maslahi yake ya kibiashara.

Mawakili hao wamemtaka Mwijaku aondoe video, machapisho na maudhui yote yanayolalamikiwa, pamoja na kutoa ahadi kwa maandishi ndani ya saa 48 kwamba hatarudia kufanya hivyo.

Aidha, Kajala kupitia mawakili wake amemtaka Mwijaku kulipa Shilingi milioni 200 ndani ya siku 14 kama fidia kwa madai ya madhara ya sifa, msongo wa kihisia, madhara ya kijamii pamoja na hasara za kiuchumi na kibiashara baada ya kusambazwa kwa video hizo na Mwijaku.

Dulla Makabila: Nikiwapima wanangu DNA, 'nitawapost'

Na Mwandishi WETU

MSANII wa Singeli nchini, Dulla Makabila ameweka wazi kuwa ana watoto wanne, lakini siku akiwapima DNA ndio atawaweka hadharani.

Msanii huyo ametoa kauli hiyo juzi alipoulizwa na waandishi wa habari kuhusu watoto wake ambao hajawahi kuweka picha zao kwenye mitandao ya kijamii.

“Nina watoto wanne, lakini kwa sasa sitawapost hadi niwapime DNA kwa sababu nimeshawahi kubambikiwa,” amesema Dulla.



Michezo ■

Tanzanite Queens mashujaa waliokosa heshima

Na John MARWA

TIMU ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania chini ya miaka 20 'Tanzanite Queens' imeaga mashindano ya Kombe la Dunia baada ya kupokea vipondo vizito kwenye fainali hizo zinazoendelea nchini Poland.

Licha ya kutolewa hatua ya makundi kwa kupokea vipigo kutoka kwa miamba ya soka duniani kama Brazil ambapo Tanzanite ilichapika mabao 4-1, huku ikichabangwa na England mabao 5-1 na dhidi ya Canada walipokea kipigo cha mabao 6-0 na kutupwa nje ya mashindano kwa kupoteza michezo yote hatua ya makundi na kuruhusu mabao 15 na kufunga mawili.

Ilikuwa mara ya kwanza Tanzanite Queens kushiriki na mara ya pili kwa timu kutoka Tanzania kushiriki Fainali za Kombe la Dunia ambapo Serengeti Girls chini ya miaka 17 walifanya hivyo na kuishia hatua ya robo fainali.

Timu za taifa kwa upande wa wanawake imekuwa na uwakilishi bora zaidi licha ya kuwa kama taifa hatujaona umuhimu wa kuwekeza katika soka la wanawake, bali kusubiri matukio ili kujionesha.

Timu hizi zimekuwa chini ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) ambao wamekuwa chachu ya mafanikio makubwa wakikosa usaidizi wa haja kwa wadau wengine nao kuichukulia kama fursa ya ajira kwa vijana wa kike nchini.

Tusingeshangaa kuona watoa hamasa wanaibuka kama Tanzanite Queens wangeendelea na mashindano, jambo ambalo halina afya zaidi ya kuzalisha wachumia tumbo wa taifa na siyo watu wazalendo wanaosimama vitani hata kama askari wameuawa.

Wino wa dhahabu kwa TFF na watendaji wote ambao wamekuwa chachu ya kuuinua mchezo wa soka la wanawake bila kujali ugumu na changamoto zilizoko mbele yao kwa maslahi mapana ya taifa na kizazi kijacho.

Tanzanite tayari wamerea nchini na hakuna hata pongezi walizopokea kama vile walivyo-pambana kivyao na TFF ndivyo ambavyo wamerejea kivyao.





Mnyama hachekeshi Afrika, Wananchi poa tu



Na John MARWA

WAWAKILISHI bora wa muda mrefu katika mashindano ya kimataifa kutoka ardhi ya Julius Kambarage Nyerere, Klabu ya Simba, hawachekeshi hata kidogo linapokuja suala la mechi za kimataifa Afrika.

Hilo limedhihirika tena jana baada ya kuwasasambua Mighty Wonders ya Malawi kwa mabao 6-1

Simba walirejea katika mitaa ya Temeke kuendeleza ubabe wao msimu huu kwa kuwa-

karibisha Mighty Wonders kwenye Dimba la Uhuru, mchezo wa mkondo wa pili wa hatua za awali ambapo wametinga kwa kishindo hatua ya mtoano kutinga makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika (CAF CL).

Jana -Septemba 13, Mnyama aliunguruma kwenye mbuga anayotamba sana kwa kutoa burudani ya kabumbu na sanaa ya kucheza na nyavu chini ya watumbuizaji bora, Clatous Chota Chama na Libasse Gueye.

Mabao ya Simba yaliwekwa kambani na Chama aliyefunga mara mbili, Libase mara mbili, huku Morice Abraham na Keletso wakiunga bao moja moja na kuwafurusha Wamawili hao kwa jumla ya mabao 7-1.

Sasa kazi inafuata salamu zinawaendea wapinzani ambao watakuwa na kibarua kizito kuja Dar es Salaam kukabiliana na joto la Jiji na pumzi ya moto ya Mnyama katika jioni za Ligi ya Mabingwa.

Wakati Simba akicheka, Wananchi, Timu ya Yanga nao walikenua Septemba 12 katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kwa kuwatupa nje Gaborone United ya Botswana kwa jumla ya mabao 3-2. Ni baada ya kushinda mabao 2-1 kwenye mtanange huo.

Ikumbukwe Simba na Yanga msimu huu zimebeba bendera ya Tanzania katika Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Azam FC na Singida Black Stars wakiwakilisha kwenye kombe la Shirikisho CAF CC.